

**KIMATAIFA** Uk. 19

## Waandishi 31 wamekwisha uawa Israel, Hamas



## Simulizi kutoka kwa mzazi na ndugu wa vijana wanaoshikiliwa Gaza

Uk. 8



**KOLAMU** Uk. 17

## Unapita njia ipi kwenye maisha?


*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

# Uelekeo




## Aziz Ki anatamba tu


Uk. 24


| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00036 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Novemba 1 - 7, 2023 |


### ZIARA YA RAIS WA UJERUMANI TZ:

# Samia, Steinmeier waibua maeneo mapya ya uchumi

- **Urejeshaji masalia ya wapendwa yanakwenda vizuri**



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa kwenye mazungumzo na mgeni wake Rais wa Jamhuri ya Shirikisho la Ujerumani, Frank-Walter Steinmeier, baada ya kuwasili Ikulu jijini Dar es Salaam jana.

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, amesema licha ya Ujerumani kuwekeza miradi 180 nchini, lakini bado kuna uwezekano mkubwa wa kukuza biashara na kwa hiyo wamekubaliana na Rais wa nchi hiyo, Frank-Walter Steinmeier, kuelekeza suala hilo katika mazungumzo yenye umuhimu kwa uchumi wa nchi mbili hizo hapo mwakani. **Uk. 4**



## Kawaid a kuzungumza na wana-CCM, wanafunzi Watanzania China

Uk.3

## Mloganzila yafanya upasuaji wenye uzito uliokithiri

Uk. 4

## Muswada Bima ya Afya watinga tena bungeni

Uk.2



## Dk. Mwinyi avitaka vikosi SMZ kuendeleza uadilifu na uwajibikaji

Uk.2

# Muswada Bima ya Afya watinga tena bungeni

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

WIZARA ya Afya inatarajiwa leo kuwasilisha tena bungeni Muswada wa Bima ya Afya kwa wote ambao ulikwama Februari, mwaka huu kwa hoja iliyotolewa na Bunge ya kutokuwepo kwa chanzo endelevu cha fedha kutekeleza mpango huo.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka Wizara ya Afya, Englibert Kayombo, muswada huo ni ndoto ya miaka mingi ya serikali.

Alisema serikali inaboresha huduma bora za afya kuanzia ngazi ya taifa hadi ya msingi kwa kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya karibu zaidi na maeneo yao.

Muswada huo utawasilishwa na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.

"Serikali kupitia Wizara ya Afya, wadau wa sekta na wataalam wengine tayari wamefanyia kazi hoja zote zilizoibuliwa na Bunge pamoja na wadau.

"Semina zimefanyika kwa makundi mbalimbali ndani ya jamii kuhusu umuhimu wa Bima ya Afya kwa wote na tulipokea maoni yao na kuyafanyia kazi, wananchi kesho (leo) wategе masikio yao Bungeni kujua nini waziri wetu atawasilisha" alisema.


Alisema kupitishwa kwa muswada huo kutawezesha kila Mtanzania kuwa ndani ya mfumo wa Bima ya Afya hatua itakayoboresha zaidi upatikanaji wa huduma za matibabu bila kuwa na kiwazo cha fedha.

"Serikali yetu ni sikivu sana na imefanyia kazi hoja zote zilizoibuliwa na wabunge ambao ndio wawakilishi waMwananchi hivyo yaliyomo ndani ya muswada huo yamelenga kuwasaidia wananchi kupata huduma bora za afya bila ya kikwazo cha fedha," alisema.

Akizungumiza kuhusu gharama za vifurushi, Kayombo alisema mara baada ya muswada huo kupita na kuwa sheria, kanuni zitatungwa ili kuratibu suala ya gharama za vifurushi, uchambuzi utafanyika ili vifurushi viwe vya gharama nafuu na kila mwananchi aweze kuwa na bima ya afya.

Akifafanua zaidi alisema, Serikali inakamilisha maandalizi ya kutoa huduma kwa wananchi kupitia mfumo wa Bima ya Afya kwa wote ambapo imeboresha ubora wa huduma katika vituo vyake vya kutolea huduma ikiwemo upatikanaji wa dawa, ununuzi na usimikaji wa vifaa na vifaa tiba, ajira za watumishi.

**Semina zimefanyika kwa makundi mbalimbali ndani ya jamii kuhusu umuhimu wa Bima ya Afya kwa wote na tulipokea maoni yao na kuyafanyia kazi, wananchi kesho (leo) wategе masikio yao Bungeni kujua...**



"Kwa sasa nchi yetu iko mbali sana katika utoaji wa huduma, tuna vifaa vya kisasa vya uchunguzi wa magonjwa, huduma nyingi za kibingwa zinapatikana hapa hapa nchini lakini pia huduma za afya zimesogezwa sana kwa wananchi hivyo kama nchi tupo tayari kutekeleza hili, nia na uwezo wa kufanya hivyo tunao," alisema.

# Sera huduma watu wenye ulemavu yapitiwa

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeanza kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2004 ili kukidhi mahitaji yaliyopo.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, alisema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Viti maalum (CCM), Stella Ikupa ambaye alihoji mkakati wa serikali kufanya marekebisho ya Sheria namba 9 ya mwaka 2010 ya Watu Wenye Ulemavu.

Akijibu swali hilo, Katambi alisema mkakati wa serikali kwa sasa ni kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu wenye Ulemavu ya Mwaka 2004 ambapo utekelezaji wake umeanza.

Aidha, alisema baada ya kukamilika kwa mapitio ya hiyo hatua za marekebisho ya Sheria zitaanza kwa kuzingatia mapungufu yatakayobainishwa katika tathmini ya utekelezaji wa sera hiyo.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti maalum (CCM), Mariam Kisangi alihoji serikali imejipangaje kutoa elimu kwa watu wenye ulemavu ili kutoa maoni kwenye mapitio hayo.

Katambi akijibu swali hilo, alisema mapitio ya sera yanatarajiwa kukamilika mwaka huu na yamekuwa shirikishi kwa makundi yote ya watu wenye ulemavu.

**Akijibu swali hilo, Katambi alisema mkakati wa serikali kwa sasa ni kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya...**

# Biteko awasilisha bungeni azimio la IRENA



**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, jana aliwasilisha bungeni mjini Dodoma azimio la kujiunga na Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu (Statute of the International Renewable Energy Agency - IRENA).

Dk. Biteko alitaja manufaa mbalimbali yatakayopatikana baada ya kujiunga na mkataba huo ikiwemo kuimarika kwa mchango wa Nishati Jadidifu katika uzalishaji wa Nishati ya Umeme nchini na kuliwezesha Taifa kuwa na vyanzo mchanyanyiko vya umeme unaoendana na mahitaji ya ukuaji wa kiuchumi na kijamii.

Alitaja manufaa mengine kuwa ni kuimarika kwa uwekezaji, mitaji na upatikanaji wa ushauri wa kiufundi katika uendelezaji wa nishati jadidifu na kupungua kwa uharibifu wa mazingira unaotokana na uzalishaji na matumizi ya nishati isiyo rafiki kwa mazingira na pia kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

# Dk. Mwinyi avitaka vikosi SMZ kuendeleza uadilifu na uwajibikaji

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

RAIS wa Zanzibar ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi, amevitaka vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuendeleza uadilifu na uwajibikaji wa majukumu yao ya kila siku.

Rais Mwinyi ambaye pia ni Kamanda Mkuu wa Idara Maalum ya vikosi vya SMZ, alitoa rai hiyo katika viwanja vya Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) Kama, wakati akizungumza na wapiganaji kwa lengo la kuwapongeza kutokana na juhudi zao za kuhakikisha amani na utulivu nchini vinaendelea kuimarishwa.

Alivitaka vikosi hivyo kuweka mbele maslahi ya nchi kwanza, uwajibikaji pamoja na kusimamia uadilifu jeshini.

Rais Dk. Mwinyi alisisitiza vikosi hivyo kuhusu suala zima la kusimamia nidhamu kwenye maeneo yao ya kazi ili kufanya kazi zao kwa uadilifu.

"Jeshi ni nidhamu ikikosekana nidhamu katika jeshi basi hapo hakuna jeshi," alisisitiza Dk. Mwinyi.

Aidha, alivipongeza vikosi hivyo kwa jitihada zao za kutoa huduma bora kwa jamii wakiwemo Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kupitia hospitali yao iliyopo Bububu pamoja na hospitali ya JKU, Saateni kwa huduma za afya wanazozitoa kwa wananchi na nyingine za jamii vikiwemo vyuo vya amali na taaluma.

Aliviagiza vikosi hivyo kuwa mfano mzuri wa kutoa huduma bora kwa raia hasa kwenye vituo vyao vya afya na taaluma vinavyohudumia jamii.

Kadhalika, aliwaagiza wakuu wa vikosi hivyo, kuendelea kusimamia uwajibikaji ili kuwe na tofauti kati ya hospitali za jeshi na za raia ili wananchi wapate huduma bora.

Pia, alivikumbusha vikosi hivyo kuwa vina jukumu la kutoa malezi bora kwa vijana na kuhakisha wanatoa vijana wazalendo wenye uchungu wa nchi yao watakaopigania maslahi ya taifa lao.

Akizungumzia suala la kuwajengea uwezo maofisa na wapiganaji wa vikosi hivyo, Rais Dk. Mwinyi aliwataka wakuu wa vikosi hivyo kuwaongezea uwezo wa kitaaluma maofisa hao kwa kuwapatia fursa za mafuzo.

Kwa upande wake Waziri wa Idara Maalum ya vikosi vya SMZ, Masoud Ali Muhammed alisema Idara Maalum ya vikosi vya SMZ zote tano ziko tayari kuetekeleza jukumu mama la kuimarisha na kuendeleza amani, utulivu na mshikamano uliopo nchini vinaendelea kusimama wakati taifa likiendeleza maendeleo ya watu wake.

Alisema Idara hizo pia zitaendelea kutekeleza maagizo, maono, mipango na fikra za Kamanda Mkuu kwa utii wa hali ya juu.

Naye Katibu Mkuu wa Idara Maalum ya SMZ, Issa Mahafoudh Haji alipongeza juhudi kubwa ya Kamanda Mkuu wa Idara Maalum ya vikosi vya SMZ, Rais Dk. Mwinyi kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa vikosi hivyo.

Alimshukuru kwa kuvishirikisha vikosi hivyo kwenye ujenzi wa miradi mikubwa ya maendeleo nchini na kueleza kuwa inawaongezea uwezo na nguvu za kiuchumi kwa kutatua baadhi ya changamoto zao.

Pia, alieleza ushiriki wao kwenye miradi hiyo, umetanua uwezo wao wa ufahamu na ujuzi wa kutekeleza majukumu yao ya kila siku pamoja na kusifu hatua ya kuwapandishia mishahara makamanda na wapiganaji kufuatia nyongeza ya mishahara aliyoitoa kwa watumishi wa umma wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar vinaundwa na Jeshi la kujenga Uchumi (JKU), (KMKM), Vikosi vya Uokozi na Zimamoto, Valantia (KVZ) na Chuo cha Mafunzo.




Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Taifa, Mohammed Kawaida, akizungumza kwenye Jukwaa la Maendeleo ya Vijana Duniani liloandaliwa na Umoja wa Vijana wa Chama Cha Kikomunisti Cha China jijini Beijing jana. Lengo la Jukwaa hilo ni kujadili na kuweka mikakati juu ya mambo yanayohusu maendeleo ya vijana duniani.
(PICHA: MPIGAPICHA WETU.)

# Kawaida kuzungumza na wana-CCM, wanafunzi Watanzania wanaosoma China

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM ya Taifa, Mohamed Kawaida, leo anatarajia kukutana na wana-CCM na wanafunzi Watanzania wanaosoma nchini China.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Idara ya Uhusiano wa Kimataifa Vyuo na Vyuo Vikuu UVCCM Taifa kwa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam jana, Kawaida atakutana na wana-CCM na wanafunzi hao Shangri-La Shougang Park, Beijing, Qunming Lake West Street, Namba 68 Shijingshan Road, Beijing, China saa 1:00 usiku kwa saa za huko.

Wakati huo huo, Kawaida jana alifanya mazungumzo kwenye Jukwaa la Maendeleo la Vijana Duniani nchini China.

# Samia, Steinmeier waibua maeneo mapya ya uchumi

Inatoka Uk. 1

Aliyasema hayo Ikulu jijini Dar es Salaam wakati mbele ya Rais wa Ujerumani, Dk. Steinmeier walipozungumza na waandishi wa habari jana.

Rais Steinmeier aliyewasili Oktoba 30, yupo nchini kwa ziara ya siku tatu.

Rais Dk. Samia alisema kufuatia mazungumzo na mgeni wake, walikubaliana kusisitiza umuhimu wa kuimarisha uhusiano wa miaka 60 kati ya nchi mbili hizo kwa manufaa ya nchi na watu wake.

"Na katika hili, tumezielekeza timu za wataalam wa nchi mbili hizi, kuendelea na mazungumzo pamoja na mashirikiano ya mara kwa mara yanayolenga kuboresha maeneo yaliyopo ya ushirikiano na kuibua maeneo mengine mapya yenye umuhimu kwa uchumi wa nchi zetu.

"Katika hili, nimemhakikishia Rais Steinmeier kwamba, Tanzania ipo tayari kuwa mwenyeji wa mazungumzo yajayo ya ushirikiano wa maendeleo yatakayofanyika mwakani," alisema.

Alitaja maeneo wanayoshirikiana na Ujerumani kuwa ni katika sekta ya afya ambapo inajenga hospitali kubwa ya Jeshi jijini Dodoma na pia imesaidia kujenga hospitali kubwa ya kisasa ya maradhi ya kuambukizwa Lugalo jijini Dar es Saalam.

Maeneo mengine ya ushirikiano ni katika elimu, elimu ya ufundi, kilimo, utalii, utamaduni na michezo, ulinzi, maliasili, hifadhi ya mazingira, udhibiti wa fedha, sekta ya maji na usambazaji wake, afya na suala la bima ya afya ambalo Tanzania ilipata usaidizi kutoka nchi hiyo.

Kuhusu utalii, Rais D. Samia alisema: "Tumekuwa tukifanya kazi kubwa sana na tunapata watalii wengi kutoka Ujerumani, lakini bado kuna uwezekano wa kupata watalii wengi zaidi pale tutakapojitangaza vizuri zaidi kwao."

Alisema Ujerumani kupitia shirika la Frankfurt Zoological Society, imekuwa ikitoa mchango mkubwa wa uhifadhi katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Hifadhi ya Taifa ya Nyerere (Selous).

"Mambo mengine tuliyozungumza ni ya kihistoria ya Tanzania wakati ule Tanganyika, na hata Zanzibar kwa muda mdogo, tulikuwa chini ya utawala wa Ujerumani, sasa katika utawala mambo mengi yamepita tumezungumza kwa urefu na tupo tayari sasa kufungua majadiliano na kuona jinsi tutakavyoweza kukubaliana kwa yale yaliyopita wakati wa utawala wa Ujerumani hapa nchini kwetu au ndani ya taifa letu vipi tufanye na ninajua kuna familia ambazo zinasubiri mabaki ya wapendwa wao ambao wako kule katika makumbusho mbalimbali ya Ujerumani, yote hayo tunakwenda kuyazungumza na kuona namna gani tunakwenda nayo vizuri," alisema.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa na mgeni wake, Rais wa Jamhuri ya Shirikisho la Ujerumani, Frank-Walter Steinmeier, baada ya kuwasili Ikulu jijini Dar es Salaam jana.

Kwa upande wake, Rais Steinmeier alisema amefurahishwa na kasi ya Rais Dk. Samia ya kujenga nchi katika mfumo wa utawala bora na wa kisheria na hivyo kuahidi kuendelea kuwa washirika wa karibu wa Tanzania.

Aidha, aliahidi kuwa Ujerumani itaendelea kuweka nchini na kudumisha ushirikiano uliopo na kuwa wenye nguvu zaidi katika maeneo kama utalii, kilimo, afya na nishati mbadala.

Alisema wataangalia namna gani wanaweza kujenga maeneo mengine ya ushirikiano kwa mfano katika kilimo, afya, matumizi ya nishati mbadala.

Ziara ya Rais Steinmeier nchini, ilimfikisha hadi Songea mkoani Ruvuma ambako alitembelea makaburi ya waathirika wa Vita vya Maji Maji na kuzungumza na vizazi vya waathirika na alizuru Makumbusho ya Kumbukumbu ya Vita vya Maji Maji.

Rais Steinmeier anarajiwa kuondoka leo kuendelea na ziara yake nchini Zambia.

## Wanne wenye uzito uliokithiri wafanyiwa upasuaji

**Aliyekuwa na uzito wa juu alikuwa na kilo 142 na aliyekuwa na uzito wa chini alikuwa na kilo 107, na kwamba tunategemea baada ya kupata huduma hii, watapungua uzito wao kwa kiasi kikubwa.**

**Na Hellen Mwango**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili Mloganzila, imefanikiwa kufanya upasuaji wa kibingwa bobezi wa kupunguza uzito kwa wagonjwa wanne wenye uzito uliokithiri kwa mara ya kwanza kufanyika nchini katika hospitali za umma.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Profesa Mohamed Janabi, alisema utaratibu huo wa matibabu, unafanyika kwa njia ya utaalamu wa hali ya juu bila upasuaji.

Profesa Janabi alifafanua kuwa wagonjwa watatu kati ya hao, wamefanyiwa kwa njia ya matundu madogo (Laparoscopic Sleeve Gastrectomy) na mmoja kwa kutumia njia ya Endoskopia (Endoscopic Sleeve Gastroplasty).

Alisema kwa kutumia endoskopia, mtu atapoteza uzito kwa asilimia 15-23 na kwa kutumia matundu madogo (Laparoscopic Sleeve Gastrectomy), atapoteza uzito kwa asilimia 50-70 ndani ya miezi 12.

"Utaratibu huu wa matibabu kwa watu wenye uzito uliopitiliza, umefanywa na Madaktari Bingwa Bobezi wa Upasuaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (Upanga na Mloganzila) kwa kushirikiana na mtaalamu bobezi wa upasuaji kutoka nchini India Dk. Mohit Bhandari pamoja na Taasisi ya Medincredi," alifafanua.

Hata hivyo, alisema kila mmoja alifanyiwa huduma hii kwa kati ya dakika 15 na 30 na kwamba watu watatu waliruhusiwa baada ya saa 24 walipokamilishiwa kupatiwa huduma hiyo na mwingine aliruhusiwa saa nane baada ya huduma hiyo.

"Aliyekuwa na uzito wa juu alikuwa na kilo 142 na aliyekuwa na uzito wa chini alikuwa na kilo 107, na kwamba tunategemea baada ya kupata huduma hii, watapungua uzito wao kwa kiasi kikubwa," alisema Profesa Janabi.

Aidha, alisema lengo ni kuhakikisha huduma hizo zinakuwa endelevu.

"Mpango wa hospitali ni kuwezesha huduma hizo kufanyika kila mwezi na kwa siku za usoni zitakuwa zinafanywa na wataalamu wa ndani," aliongeza.

Profesa Janabi alisema pia wanatoa huduma mbalimbali za kibingwa bobezi ikiwamo kupandikiza figo, kupunguza uzito kwa kutumia puto maalum (intra gastric balloon), kuondoa uvimbe kwenye sakafu ya ubongo kwa matundu ya pua, kuvunja mawe kwenye figo kwa kutumia mawimbi mtetemo, kupandikiza nyonga bandia na upasuaji wa kutumia matundu madogo.

Alimpongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuwekeza katika sekta ya afya ikiwamo kununua vifaa tiba kuanzia ngazi ya zahanati hadi kwenye hospitali bobezi ya Taifa na kumpunguzia gharama mgonjwa kutafuta tiba nje ya mipaka ya nchi.

"Wote mnaelewa changamoto ya fedha za kigeni, hawa tusingewafanyia upasuaji hapa, wangetafuta njia moja au nyingine kwenda nje maana yake wangetumia fedha za kigeni," alisema.



Baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Magula Kata ya Sitalike Wilaya ya Mpanda mkoani Katavi, wakiwa katika moja ya eneo la vituo vya kuchotea maji (DPS) vilivyojengwa kupitia mradi wa maji Magula uliokamiliki kwa gharama ya Sh. milioni 545 na Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini

# Magula wakamilishiwa mradi wa maji mil. 545/-

**Na Mwandishi Wetu, Katavi**

WANANCHI wa Kijiji cha Magula Kata ya Sitalike Wilaya ya Mpanda mkoani Katavi, wamepata ahueni baada ya kukamilika kwa mradi wa maji safi na salama ya bomba uliogharimu Sh. milioni 545.

Kabla ya kukamilika kwa mradi huo, wananchi hao wakisafiri masafa marefu kutafuta huduma hiyo, hali iliyotishia usalama wa maisha yao na wanyama wakali wakiwemo simba.

Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassam, kupitia Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa) kukamilisha ujenzi wa mradi wa maji ya bomba uliogharimu Sh.milioni 545 katika kijiji hicho.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wananchi wa Kijiji cha Magula walisema,kabla ya kukamilika kwa mradi huo, maisha yao yalikuwa hatarini kwa kushambuliwa na wengine kuuawa na wanyama hao pindi wanapokwenda kufuata maji kwenye mto na vyanzo vingine vilivyopo katika Hifadhi ya Taifa ya Katavi.

> **Kabla ya kukamilika kwa mradi huo, wananchi hao wakisafiri masafa marefu kutafuta huduma hiyo, hali iliyotishia usalama wa maisha yao ...**

Rosse Joseph, alisema kukamilika kwa mradi huo ni jambo la faraja kwa sababu wameondokana na hatari ya kuendelea kuliwa na wanyama hao na kuishukuru serikali kwa uamuzi wa kuwajengea mradi wa maji ya bomba.

Naye Noel Cletus, alisema sasa wananchi wa kijiji hicho wana furaha na amani kubwa kutokana na huduma ya maji safi na salama kupatikana kila mtaa ,hivyo kutoa fursa na kwao kujikita katika shughuli za maendeleo badala ya kutumia muda mwingi kwenda kutafuta maji.

# ‘Vunja ndoa hii... ananiona takataka’

**Na Zawadi Kapambwe, Mbeya**

GIDEON Siame (32), mkazi wa Soweto Agape, jijini Mbeya, ameitaka mahakama kuvunjilia mbali ndoa yake, akidai mkewe anamdharau na amekuwa si mwaminifu kwenye ndoa yao.

Amezidi kudai kwamba, kama hilo halitoshi, mkewe huyo, Wiven Simkonda (30), amekua akitoroka mara kwa mara na kumwachia watoto.

“Mheshimiwa hakimu, huyu mwanamke nimekosa uaminifi tena kwake kutokana na dharau anazonionesha.

Alikofikia, dharau zake haziwezi kurekebishika (na hivyo, siwezi kuendelea kuishi na mwanamke kama huyu),” alisema Gideon ambaye ndiye mdai wa talaka katika shauri hilo.

Mdai huyo alisema kuwa baada ya kufunga ndoa ya kimila na mke wake miaka kadhaa iliyopita, walibahatika kupata watoto watatu na maisha yalikuwa yanakwenda vizuri.

Alisema baada ya muda, akashangaa kuona mkewe anabadilika na kuanza kumdharau na kumwasi kwa kuanzisha mahusiano na mwanaume mwingine.

“Pengine ni kutokana na kunogewa penzi la huyo mwanaume, amekuwa na kiburi na dharau zilizokithirimbele yangu. Yaani mimi ni takataka, hajali kabisa kwamba huyu ni nimume wangu wa ndoa,” alisema.

> **Pengine ni kutokana na kunogewa penzi la huyo mwanaume, amekuwa na kiburi na dharau zilizokithirimbele yangu. Yaani mimi ni takataka, hajali kabisa...**

Aliendelea kuieleza mahakama kuwa yeye na Wiven walikua wakishirikiana mambo mbalimbali ya kimaendeleo ikiwemo biashara alizokua akifanya mkewe kabla ya kubadilika na kuwa mithili ya kichomi.

“Mheshimiwa Hakimu, naomba vunja ndoa hii, kwani baada ya uchunguzi wangu wa kina nimegundua kuwa mke wangu hanipendi tena kwa sababu mambo yake mengi anafanya mwenyewe. Hataki hata kunishirikisha.

Sasa katika mazingira kama hayo utasema huyu ni mke wa kufanya nae maisha?" Alihoji mdai.

Gideon alikua akitoa madai yake kwenye kesi hiyo ya talàka anayomlalamikia mkewe kwa kushindwa kutimiza majukumu yake kama mke, mbele ya hakimu Miriam Kamwaga wa mahakama ya Mwanzo Mjini Mbeya.

Mdaiwa kwa upande wake alisema kuna sababu za msingi zilizopelekea yeye kufanya maamuzi magumu kama hayo.

Alisema hiyo ni baada kuthibitisha kwamba mumewe anachepuka nje ya ndoa kiasi cha kuzaa mtoto.

Kesi hiyo imeahirishwa na itakuja tena mahakamani hapo Novemba 9 mwaka huu kwa ajili ya hukumu.

# Adai kuchoshwa na mume, asubiria kwa hamu

**Na Zawadi Kapambwe, Mbeya**

MDAIWA katika kesi ya madai ya talaka, Mariana Mwambenja (25), ameieleza mahakama kuwa amechoshwa na tabia ya mumewe hivyo yupo tayari kupokea talaka hiyo aliyokuwa akiisubiria kwa bashasha.

“Yaani hiyo talaka nilikuwa naitafuta, sikujua wapi naweza kuipata... maadamu yeye ndio amenileta hapa, nami nipo tayari kuopokea talaka hiyo sababu mwanaume anaghubu huyu, kila iitwapo leo na kipigo kisichoisha,” alisema.

Mariana mkazi wa Ilembo jijini hapa alidai kuwa migogoro kati yake na mumewe ilianza mara baada mumewe kupata mwanamke mwingine.

“Kiukweli huyu kaka nimemchoka, sihitaji hata kumuona hivyo, Mheshimiwa Hakimu toa tu hiyo talaka ili kila mtu achukue hamsini zake, kwanza sihitaji hata kuona sura yake," alidai.

Awali mdai Anajua Petrol (32) alifika mahakamani akiomba mahakama kuvunja ndoa yake kwa madai kuwa alitelekezwa na mkewe muda mrefu bila huduma yoyote wala kupatiwa tendo la ndoa.

Mdai alitoa madai yake mbele ya Hakimu Nitike Kiputa wa Mahakama ya Mwanzo Mjini ambayealiahirisha kesi hiyo hadi Novemba 10, mwaka huu itakapotajwa.

> **Yaani hiyo talaka nilikuwa naitafuta, sikujua wapi naweza kuipata...maadamu yeye ndio amenileta hapa, nami nipo...**

# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO

### Kumwaga, kutitirisha ovyo uchafu



BAADHI ya watu, kwa kutojali afya za wengine, wamekuwa na tabia ya kumwaga taka ngumu au kutiririsha majitaka mitaani. Watu hawa hawajali kama ni barabara wanamopita watu, ni makazi ya watu au maeneo ya biashara. Wao ni kumwaga tu waondoe udhia kwenye maeneo yao.

Hawa ni watu ambao ni hatari na hivyo hatuna sababu ya kuwachekea na kuwavumilia. Tuwafikishe kwenye taasisi za kisheria tukiwang'amua ili wachukuliwe hatua. Waswahili wanasema ukicheka na nyani utavuna mabua.




## MAONI YA MHARIRI

# Tanzania, Ujerumani zipo fursa nyingi za ushirikiano

JANA, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, alikutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Ujerumani, Frank-Walter Steinmeier.

Mazungumzo ya Viongozi hawa pamoja na mambo mengine, yalijikita zaidi jinsi ya kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi kwa maslahi mapana ya wananchi wa nchi hizo mbili.

Rais Dk. Samia kwa upande wake, alisema licha ya Ujerumani kuwekeza miradi 180 nchini, lakini bado kuna uwezekano mkubwa wa kukuza biashara na kwa hiyo wamekubaliana kuelekeza suala hilo katika mazungumzo yenye umuhimu kwa uchumi wa nchi mbili hizo hapo mwakani.

Rais Steinmeier aliyewasili Oktoba 30, yupo nchini kwa ziara ya siku tatu.

Rais Dk. Samia alisema wamekubaliana na Rais Steinmeier kusisitiza umuhimu wa kuimarisha uhusiano wa miaka 60 kati ya nchi mbili hizo kwa manufaa ya nchi na watu wake.

Hivyo, alisema kwa mantiki hiyo, wamezielekeza timu za wataalam wa nchi hizo, kuendelea na mazungumzo pamoja na mashirikiano ya mara kwa mara yanayolenga kuboresha maeneo yaliyopo ya ushirikiano na kuibua maeneo mengine mapya yenye umuhimu kwa uchumi wa Tanzania na Ujerumani.

Ni makubaliano mazuri yanayolenga kuzidisha uhusiano mzuri kati ya mataifa haya mawili.

Uhusiano wa Tanzania na Ujerumani, ni wa kihistoria katika sekta mbalimbali ikiwemo ya afya, hivyo ni muhimu uendelee kudumishwa kwa faida ya watu wa nchi hizo mbili.

Kwa mfano, tayari Ujerumani inajenga hospitali kubwa ya Jeshi jijini Dodoma na pia imesaidia kujenga hospitali kubwa ya kisasa ya maradhi ya kuambukizwa Lugalo jijini Dar es Saalam.

Yapo pia maeneo mengine ya ushirikiano katika elimu, elimu ya ufundi, kilimo, utalii, utamaduni, michezo, ulinzi, maliasili, hifadhi ya mazingira, udhibiti wa fedha na sekta ya maji.

Aidha, katika sekta utalii, Tanzania imekuwa ikipata watalii wengi kutoka Ujerumani, lakini bado kuna uwezekano wa kupata watalii wengi zaidi.

UELEKEO kwa dhati kabisa, inaungana na viongozi wakuu hawa katika kuhakikisha kwamba suala la ushirikiano kwenye maeneo hayo tajwa na mengine kadha wa kadha, ni jambo la muhimu kwa ustawi wa wananchi wa Tanzania na Ujerumani.


## Wasiliana nasi

**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000
**Mhariri wa Habari:** +255768411003
**Mhariri Michezo:** +255787559090
**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825
**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam
**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro
**Jengo la:** Aura Mall
**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532
**Email:** uelekeohabari@gmail.com




Na Godfrey Sanga
JICHO LANGU
Sangagodfrey26@gmail.com

# Tukuze diplomasia ya uchumi, tunyanyue nchi

DIPLOMASIA ni sanaa, sayansi na njia ambazo mataifa, vikundi, au watu binafsi huendesha mambo yao kwa njia zinazolenga kulinda masilahi yao na kukuza uhusiano wao wa kisiasa, kiuchumi, kitamaduni au kisayansi. Hayo yanafanyika huku wakidumisha uhusiano wenye amani.

Kwa muda mrefu tangu kupata uhuru, nchi zetu ikiwemo Tanzania, linapokuja suala la diplomasia, zilijikita zaidi katika kuendesha uhusiano wa kisiasa, yaani diplomasia ya kisiasa.

Katika muktadha huo, mambo mengi yaliangaliwa hususani kuzuia nchi na nchi kuingia katika machafuko. Kwa hiyo diplomasia ya kisiasa imesaidia sana katika kutatua migogoro ya nchi na nchi na kusimamisha vita au michafuko yoyote na hivyo kuleta amani na utulivu katika dunia yetu.

Kwa mfano, dunia kwa sasa inashuhudia vita baina ya Urusi na Ukraine huku nchi mbalimbali zikijaribu kutafuta suluhu kwa njia ya diplomasia.

Pia kuna vita baina ya wanamgambo wa Hamas na majeshi ya Israel vinavyoendelea, vita ambavyo kupitia diplomasia ya uchumi vinaweza kukoma.

Kwa kuwa nchi yetu, Alhamdulillah, ina amani, katika miaka ya karibuni, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, imekuwa ikijielekeza zaidi kwenye diplomasia ya huchumi. Hii ni nini hasa?

Diplomasia ya uchumi ni jinsi nchi zinavyotumia sera za nje kujenga nguvu za kiuchumi na ustawi nyumbani.

Kupitia diplomasia ya uchumi wawakilishi wetu katika mataifa mbalimbali kwa maana ya mabalozi walioko nje ya nchi wanategemewa kufanya diplomasia ya uchumi kwa hali na mali. Wasibweteke.

Kikubwa wanapaswa kuvutia wawekezaji kuja kuwekeza katika nchi yetu yenye neema nyingi. Tuna neema ya raslimali watu, ardhi, madini, mbuga za wanyama, mito, maziwa na kadhalika.

Mbali na kuwa na raslimali hizo, Tanzania ni nchi ya amani na watu wengi ni waungwana sana. Haya ni mambo ambayo wageni wanapaswa kujua. Wanapaswa pia kujua wapi wanaweza kuwekeza na kwenye nini. Wanapaswa kujua sera zetu za uwekezaji ambazo kimsingi ni nzuri sana.

Pamoja na hili wawakilishi wetu kupitia diplomasia ya uchumi wanapaswa kuwawezesha Watanzania kujua fursa zinazopatikana huko waliko.

Mabalozi watusaidie katika kushiriki mikutano, makongamano na maonesho ya biashara ndani na nje ya nchi.

> **Kwa kuwa nchi yetu, Alhamdulillah, ina amani, katika miaka ya karibuni, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, imekuwa ikijielekeza zaidi kwenye diplomasia ya huchumi.**

Kwa upande wa ndani, moja ya maonesho nchini mwetu ambayo tunataka kuona wageni wengi wakija ni ya Sabasaba na Nanenane. Ikumbukwe pale katika viwanja vya John Mwakangale, Mbeya sasa ni maonesho ya kimataifa ya Nanenane.

Katika kukuza diplomasia ya uchumi, kwa maana ya kutangaza vivutio vya uwekezaji tulivyo navyo sambamba na Watanzania kujua na hatimaye kupata fursa zinazopatikana nje, inatakiwa hii isiwe kazi ya serikali au mabalozi pekee. Kila mtanzania mwenye nafasi ana dhima hiyo.

Kazi Iendelee.

# Waonja maji ya bomba kwa mara kwanza tangu Tanzania ipate Uhuru

**Na Mwandishi Wetu, Katavi**

WAKAZI wa Kijiji cha Vikonge Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi, kwa mara ya kwanza tangu Uhuru, wameanza kupata na kutumia maji safi na salama ya bomba.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa), kukamilisha ujenzi wa mradi wa maji katika kijiji hicho.

Meneja wa Ruwasa Wilaya ya Tanganyika, Alkam Sabuni, alisema mradi huo unahudumia jumla ya wakazi 8,400 na umegharimu Sh. milioni 608 na umeanza kutoa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi.

Sabuni alisema utekelezaji wa mradi huo, umehusisha ujenzi wa tangi la kuhifadhi maji lita 100,000 vituo vya kuchotea maji 31 ambavyo vyote vimekamilika na vinatoa huduma na kujenga miundombinu mingine.

Alifafanua kuwa kupitia mradi huo, Ruwasa imeanzisha chombo cha watumia maji ngazi ya jamii (CBWSO) inayofahamika kwa jina la Mpakato ambacho kinahudumia vijiji 11 ambapo kati ya hivyo, vijiji tisa vinapata maji ya bomba na viwili vinapata maji kupitia visima vya kusukuma kwa mkono.

Aidha, alisema kabla ya kuanzishwa kwa Ruwasa mwaka 2019, hali ya upatikanaji wa maji katika Wilaya ya Tanganyika, ilikuwa asilimia 65, lakini katika kipindi kifupi cha miaka mitatu cha Ruwasa, upatikanaji wa huduma ya maji imefikia asilimia 81.

"Kati ya watu 375,000 wa Wilaya ya Tanganyika, zaidi ya watu 330,000 wanapata huduma ya maji safi na salama kupitia vituo vya kuchotea maji (DPS) na ndani ya nyumba zao, hivyo kutimiza kwa vitendo lengo la Rais wetu, Dk. Samia Suluhu Hassan, ya kumtua mama ndoo kichwani" alisema Sabuni.

Alisema Wilaya ya Tanganyika yenye jumla ya watu 375,000 ina vijiji 55 na kata 16, kati ya vijiji hivyo, 39 vimefikiwa na huduma ya maji safi na salama ya bomba.

Pia alisema kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ruwasa inaendelea kutekeleza miradi minane yenye thamani ya Sh. bilioni 7.9 ambayo utekelezaji wake uko katika hatua mbalimbali na baadhi ya miradi hiyo imeanza kutoa huduma kwa wananchi licha ya kutokamilika kwa asilimia 100.

Alisema ifikapo Desemba 30, mwaka huu, miradi hiyo itakamilika na kuongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika wilaya hiyo kutoka asilimia 81 hadi asilimia 86, hivyo kuvuka lengo la kitaifa la asilimia 85 kwa maeneo ya vijijini.

Katika hatua nyingine, Sabuni alisema kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Ruwasa Wilaya ya Tanganyika, imepangiwa kutumia Sh. bilioni nne kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji katika vijiji vinne.

Sabuni alieleza kuwa, vijiji hivyo ni kati ya vijiji 16 ambavyo bado havijafikiwa na mtandao wa maji ya bomba na miradi hiyo itakapokamilika itaongeza upatikanaji wa maji kutoka asilimia 86 hadi kufikia asilimia 92 mwaka 2024.

Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika, Onesmo Busweru, alimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuipatia wilaya hiyo zaidi ya Sh. bilioni tisa ambazo zimetumika kutekeleza miradi ya maji katika vijiji mbalimbali.

Alisema fedha hizo zimetumika kuimarisha na kuboresha huduma ya maji safi na salama na kuwataka wananchi kuhakikisha wanaunga mkono jitihada za serikali kwa kulinda miundombinu na miradi ya maji inayotekelezwa katika maeneo yao.

Mkazi wa Kijiji cha Vikonge Anna Peter, aliipongeza serikali kwa kuwaleta mradi huo ambao umemaliza kabisa changamoto ya huduma ya maji safi na salama.

Alisema awali, hali ya upatikanaji wa maji safi na salama haikuwa nzuri kwani walitumia maji ya visima vilivyochimbwa enzi za ukoloni, lakini hata hivyo havikutosheleza mahitaji yao kutokana na idadi kubwa ya watu kijijini hapo.



# Ajuza auawa kikatili imani za kishirikina

**Na Mwandishi Wetu, Njombe**

AJUZA mwenye umri wa miaka 80, Zainab Mkupasi, mkazi wa Kijiji cha Mbembe Wilaya ya Wanging'ombe mkoani Njombe, amekutwa ameuawa kwa kupigwa na kiti cha miguu mitatu (kigoda) na watu ambao bado hawajafahamika.

Hata hivyo, chanzo cha mauaji hayo kinadaiwa kuwa imani za kishirikina.

Kwa mujibu wa taarifa za awali za Polisi wilayani Wanging'ombe, kabla ajuza huyo hajakutwa na umauti, wanafamilia ya mzee Mkupasi walishiriki kikao cha pamoja kilichojadili suala la ushirikina wakimtuhumu bibi huyo.

Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Claudia Kitta, alikemea dhana ya imani potofu kwa baadhi ya vijana wilayani humo kutofanya shughuli za maendeleo kwa kuhofia ushirikina.

"Mheshimiwa Rais Samia alituagiza kusimamia amani kwenye maeneo yetu ndiyo maana nimefika hapa Mbembe hii ni mara ya pili, diwani alisema matukio kama haya mmeanza muda mrefu sana kwenye kijiji hiki ni aibu," alisema Kitta.

**Mheshimiwa Rais Samia alituagiza kusimamia amani kwenye maeneo yetu ndiyo maana nimefika hapa Mbembe hii ni mara ya pili, diwani alisema matukio kama haya mmeanza muda mrefu sana kwenye kijiji hiki ni aibu.**

# Polisi wasaka walioua mtuhumiwa

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi Mkoa wa Mwanza, linawatafuta watu waliojichukulia sheria mkononi kwa kuwaua watu wawili kwa kuwashambulia na mawe na silaha za jadi wakiwatuhumu kuiba gunia moja la mpunga.

Akizungumza na nanahabari jana, Kamanda wa Polisi mkoani humo Wilbroad Mutafungwa, alisema tukio hilo lilitokea Oktoba 30, mwaka huu katika Kijiji na Kata ya Mwaniko wilayani Misungwi na kuwataja waliouawa kuwa ni Nkula Lameck (26), mkazi wa Mwamanga na Nzuri Kazungu (25), mkazi Inchobela wilayani Magu.

Kamanda Mutafungwa alisema watu hao waliojichukulia sheria mkononi wakiwatuhumu kuiba gunia moja la mpunga.



"Inadaiwa Nkula na mwenzake Nzuri, walikuwa wamebeba mpunga kwenye pikipiki yenye namba za usajili MC 989 CWU aina ya Kinglion iliyochomwa moto na kuteketea kabisa wakati wa tukio hilo wakitokea Kijiji cha Budulana Ngufu wilayani Kwimba na walipofika Kijiji cha Mwaniko wilayani Misungwi, ndipo walipozuiliwa na kuuawa na watu hao," alifafanua Kamanda Mtafungwa.

# Simulizi za kusikitisha kutoka kwa mzazi na ndugu wa vijana wanaoshikiliwa Gaza

**Na Mwandishi wa BBC.**



Joshua Loitu



Clemence Felix

BABA na baadhi ya ndugu wa Watanzania wawili wanaoshikiliwa mateka na wanamgambo wa Hamas huko Gaza, wanatoa simulizi kuhusiana na kukosa mawasiliano na vijana wao wawili, Joshua Loitu na Clemence Felix Mtenga.

Wawili hao ni wanafunzi wa mafunzo ya kilimo kwa vitendo. Walitekwa Oktoba 7, mwaka huu wakati wa mashambulio ya Hamas kwa Israel kisha nchi hiyo kuanzisha mashambulizi ya kulipa kisasi.

**BABA MZAZI WA JOSHUA;**

Loitu Mollel, ambaye ni baba mzazi wa Joshua, anaeleza kwa vyombo vya habari kwamba, kijana wake alikwenda Israel Septemba 18, mwaka huu kwa ajili ya masomo kwa vitendo.

xAnasema alikuwa anawasiliana naye vizuri siku zote: "Mara ya mwisho nimewasiliana na mwanangu Oktoba 5, mwaka huu, lakini pia mara ya mwisho nilimuona hewani kwenye whatsApp 'online' Oktoba 7, mwaka huu saa nne na dakika tatu ya asubuhi. Kwa kweli sina raha kabisa," anasema na kuongeza:

"Sina raha, familia yote hatuna raha kwa sababu hatumpati huyu kijana kwenye simu, mke wangu na ndugu zangu, wanataka niongeze jitihada ili kufahamu alipo na yupo katika hali gani. Jitihada ninazoendelea nazo kufuatilia kupitia kwa Ubalozi wa Tanzania nchini Israel licha ya kuwa na wao wamenieleza kuwa wanaendelea kufuatilia kufahamu alipo kijana wangu," anasema Mollel.

Mollel anaeleza kuwa hafahamu Joshua ambaye ni mwanawe kati ya watoto wake watano, yuko katika hali gani na kwamba anasubiri taarifa kutoka kwenye mamlaka za Tanzania.

Hatua ya kufuatilia alipo kijana wake inakuja siku kadhaa baada ya Ubalozi wa Tanzania nchini Israel kusema kwamba hauna mawasiliano na raia wawili wa nchi hiyo ambao wanaishi eneo la Kusini mwa nchi hiyo ambalo lilishuhudia mapambano baina ya wanamgambo wa Kipalestina wa Hamas pamoja na Jeshi la Israel.

Ubalozi wa Tanzania ulisema kuwa bado haujafanikiwa kuwasiliana na vijana ambao walidai kutokuwa na mawasiliano nao.

Hivi karibuni, Ubalozi wa Tanzania nchini Israel, uliwarudisha Watanzania tisa waliokuwa nchini humo, hata hivyo, bado wengine zaidi ya raia 350 wanaendelea kuishi katika maeneo mbalimbali nchini Israel.

**DADA WA CLEMENCE**

Kwa upande wake, Neema Christina Mtenga ambaye ni dada wa Clemence, anasema familia ina matumaini mapya baada ya kusikia majina ya waliotekwa akiwamo ndugu yao kuliko awali waliposhindwa kufahamu mahali alipo, bado wana hofu, lakini wana uhakika yuko hai.



Neema

**Tulipozungumza na Ubalozi, tumepata taarifa za matumaini kwamba yupo, lakini siwezi kusema kwamba tuna ahueni sana tofauti na awali. Balozi wa Tanzania aliyepo Israel, aliwasiliana na baba yetu na alichotuambia ni kwamba Clemence ni mmoja wa watu ambao hawaonekani na kuna namna ambavyo anafanya ili kumpata.**

"Tulipozungumza na Ubalozi, tumepata taarifa za matumaini kwamba yupo, lakini siwezi kusema kwamba tuna ahueni sana tofauti na awali. Balozi wa Tanzania aliyepo Israel, aliwasiliana na baba yetu na alichotuambia ni kwamba Clemence ni mmoja wa watu ambao hawaonekani na kuna namna ambavyo anafanya ili kumpata," anasema.

"Kwa sasa, kila mtu ana shaka, huzuni, ukizingatia kuwa ni mdogo wetu na ni juzi tu alikwenda na hali ukiangalia katika vyombo vya habari inatia shaka, hakuna mtu ambaye anaweza kulala vizuri. Kwa kweli sijui nielezeje, lakini ni hivyo," anaeleza na kuongeza:

"Tunaamini kwamba kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, watarejea kulingana na taarifa tunazopata kupitia machapisho mbalimbali kwani miongoni mwa waliotekwa na Hamas, kwa hiyo tunaamini kwamba kwa huruma ya Mungu, ndugu yetu atarejea salama," anasimuliza Mtenga.

Akimzungumzia Clemence kitabia na mwenendo anasema ni mtulivu, anayefanya mambo yake kwa umakini pia mtaratibu na kwa sababu ya utulivu huo, ndiyo maana wanapata shaka juu ya hali yake huko aliko kwa sasa na kwamba wangependa apate ujumbe kuwa wanampenda na wanamuombea usiku na mchana.

Mapema wiki iliyopita, Serikali ya Israel ilithibitisha utambulisho wa watu wawili kutoka Tanzania wanaoaminika kushikiliwa na Hamas tangu shambulio la Oktoba 7, mwaka huu dhidi ya jamii za Kusini mwa Israel, karibu na mpaka na Gaza.

Watanzania hao walitajwa kuwa ni Joshua na Clemence walikuwa nchini humo kama sehemu ya programu ya mafunzo ya kilimo, kulingana na taarifa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje ya Israel.

"Walitekwa nyara na magaidi wa Hamas na wanazuiliwa mateka huko Gaza," ujumbe huo ulisema. "Tafadhali ungana nasi kuwaombea warudi salama na mara moja."

Joshua na Clemence, walikuwa sehemu ya kundi la wanafunzi waliokuwa wakiishi Kibbutz Nahal Oz. Walikuwa wametoweka tangu mashambulizi hayo, lakini Israel ilikuwa bado haijathibitisha utambulisho wao au kuripoti kilichowapata.

Hata hivyo, Alhamis iliyopita, Serikali ya Tanzania ilisema kuwa inafahamu kuhusu wanafunzi wawili waliopotea ambao ni sehemu ya kundi la Watanzania 260 nchini Israel, lakini bado haijathibitisha walipo. Hata hivyo, Watanzania tisa waliokuwa Israel walirejea nyumbani Oktoba 18, mwaka huu.

Vyombo vya habari, vilizungumza na Joshua Mollel, ambaye ni mmoja wa mwanafunzi hao, lakini vikasema havikuwa vimewasiliana naye tangu wakati wa shambulio hilo.

Habari hizo zinakuja huku kukiwa na majadiliano ya pendekezo la Hamas la kuwaachilia mateka. Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, Hossein Amirabdollahian, alisema wiki iliyopita kwamba Hamas iko tayari kuwaachilia mateka, lakini; "ulimwengu unapaswa kuunga mkono kuachiliwa kwa Wapalestina 6,000" ambao wamekuwa wakishikiliwa katika jela za Israel.

"Viongozi wa vuguvugu la ukombozi la Hamas, wametangaza kuwa tayari kuwaachilia wafungwa wasiokuwa wanajeshi na Iran, Uturuki na Qatar ziko tayari kutekeleza jukumu lao katika juhudi hii muhimu," alisema mwanadiplomasia huyo wa Iran.

Ubalozi wa Israel mjini Pretoria awali uliripoti kuwa raia wawili wa Afrika Kusini, raia wa Eritrea na raia mmoja wa Sudan, pia walikuwa miongoni mwa waliofariki dunia au kutoweka.

Mapema Oktoba 23. mwaka huu, ilibainika kuwa Watanzania wawili na raia mmoja wa Kusini ni miongoni mwa mateka 224 wanaoshikiliwa na Hamas baada ya mashambulizi ya Oktoba 7, mwaka huu.

Balozi wa Tanzania nchini Israel, Alex Kallua, alivieleza vyombo vya habari kuwa ofisi yake pia imepata uthibitisho kutoka kwa mamlaka za Israel kuwa raia wawili wa Tanzania ni mateka wa Hamas.

Balozi Kallua pia hakuthibitisha kama mateka hao ndiyo wale wale wanafunzi wawili ambao hapo awali ofisi yake iliripoti kuwa hawajulikani walipo.

Mwandishi wa makala hii alizungumza na familia ya mmoja wao, Joshua, ambaye alikuwa mwanafunzi wa kilimo kwenye mojawapo ya eneo la makazi lililolengwa .

Wageni kutoka nchi 25 kwa jumla wanazuiliwa na Hamas, Israel inasema, walichukuliwa wakati wanamgambo kutoka Hamas - ambayo Israel, Uingereza, Marekani na kundi la mataifa yenye nguvu, yanaitaja kama shirika la kigaidi - walipovuka hadi Israel kutoka Gaza na kuua takriban watu 1,400.

Israel tangu wakati huo imelipiza kisasi kwa mashambulizi ya anga huko Gaza, ambayo Wizara ya Afya inayoendeshwa na Hamas, inasema yameua takriban watu 6,500.

Jarida hili haliuzwi

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA

| Jumatano Novemba 1 - 7, 2023 |

# Jungu kuu















# Tuwajenge na kuwaibua kina Dk Tulia wengi zaidi

UK. 12 & 13

Siasa

Na Reubeni Lumbagala, Kongwa

# Wazazi, zingatieni ushauri wa Jokate malezi ya watoto

MMOMONYOKO wa maadili, ni tatizo linaloikabili nchi yetu na maeneo mengine ulimwenguni. Mmomonyoko huu unahatarisha mustakabali mwema wa kizazi cha sasa na kijacho kwani uwepo wa vitendo vinavyokwenda kinyume cha maadili, mila, desturi na taratibu za nchi yetu, si tu vinavunja tamaduni zetu, bali pia ni adui wa maendeleo ya nchi yetu.

Ni dhahiri shahiri kuwa hatua stahiki zinapaswa kuchukuliwa kuanzia ngazi ya familia, jamii na nchi kwa ujumla ili kunusuru mmomonyoko wa maadili unaohatarisha kila nyanja ya maisha kisiasa, kiuchumi na kijamii. Wazazi na walezi ni wadau muhimu katika mapambano haya ya mmomonyoko wa maadili.

Ni ukweli kuwa hakuna namna ambayo wazazi na walezi wanaweza kujitenga na mmomonyoko wa maadili ya watoto unaoonekana leo hasa kuanzia ngazi ya familia.

**Wazazi wanatakiwa kushika nafasi zao za ulezi na kuongoza watoto na kuwasaidia, kipindi hiki tunaona wazazi wanawaogopa...**

Katika saikolojia ya makuzi ya watoto inaaminika kuwa, kila mtoto anayezaliwa huwa ana tabia njema ila jamii anayokutana nayo ndiyo inaamua kama ataendelea kuwa mtoto mwenye tabia njema (proper behaviour) au tabia mbaya (improper behaviour).

Iko hivi: Mtoto anapozaliwa huwa hajui kutukana, kuiba, kudharau watu wala aina yoyote ya tabia mbaya, kwani mtoto huzaliwa akiwa na tabia njema isiyo na mawaa kabisa. Makuzi anayopata mtoto kuanzia katika familia na jamii inayomzunguka huwa ndiyo yenye kutoa mwelekeo wa aina ya tabia na maadili ya mtoto kama maadili yawe mazuri au mabaya. Hivyo basi, malezi bora kuanzia ngazi ya familia ni muhimu sana katika kujenga tabia njema ya mtoto. Maandiko Matakatifu katika Biblia, kitabu cha Mithali 22:6, Biblia inasema, "Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee."

Kutokana na ukweli kuwa mtoto huzaliwa akiwa na tabia njema na maadili mazuri, mlolongo huo unapaswakuendelezwa pindi tu anapozaliwa hadi ukuaji wake wote.

Ndiyo maana Maandiko Matakatifu yanasisitiza kuwa mzazi anawajibika kumlea mtoto katika njia nzuri na msingi huo utakaowekwa na mzazi au mlezi, utamsaidia mtoto kuendelea na tabia njema hiyo si tu katika utoto wake bali hata katika ujana, utu uzima na uzee wake wote.

Ewe mzazi au mlezi ambaye hujasikia ujumbe wa Jokate Mwegelo, basi hujachelewa, ujumbe wenyewe huu hapa.

Oktoba 27, mwaka huu, Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Jokate Mwegelo, akizungumza na wanahabari, alisisitiza suala la maadili kwa watoto akiwataka wazazi kutimiza wajibu wao usiokwepeka wa kuwalea watoto katika maadili mazuri ili kuwa na viongozi bora katika jamii.



Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Jokate Mwegelo



"Wazazi wanatakiwa kushika nafasi zao za ulezi na kuongoza watoto na kuwasaidia, kipindi hiki tunaona wazazi wanawaogopa watoto kuliko watoto wanavyowaogopa," amesema Jokate.

Alichosema Jokate ni jambo la kweli kabisa. Kuyumba kwa maadili ya watoto kumechangiwa pia na baadhi ya wazazi kushindwa kubeba majukumu yao kikamilifu ya malezi na hivyo watoto kujiongoza wenyewe. Tumefikia hatua mbaya ambapo mzazi anaogopa kukemea tabia mbaya anazoziona kwa mtoto/watoto wake. Mathalani, mtoto anaweza kuwa anafanya vitendo vya wizi, kutumia dawa za kulevya, kuuza mwili wake (ukahaba), na mengine mengi, lakini mzazi au mlezi akafumbia macho vitendo hivi na wakati mwingine kuwa mtetezi wa mtoto wake pindi anapopewa taarifa za tabia mbaya dhidi ya mtoto wake.

Pia, baadhi ya wazazi na walezi hawana muda kabisa wa kuongea na watoto wao, kujua changamoto zao na namnaya kuzitatua. Ni muhimu kwa mzazi kuwa na muda wa kutosha wa kuongea na watoto wake ili watoto wajue yale wanayayopenda wazazi wao na yapi hawayapendi. Ni muhimu kupandikiza maadili na tabia njema kwa watoto ili wakue wakiyaishi yale waliyofunzwa na wazazi wao.

Tukifanikiwa kujenga maadili mema katika ngazi ya familia, hata nchi itakuwa na raia wema kwani watoto ni raia pia. Mafanikio ya malezi mazuri katika familia yanaleta manufaa ya kupata viongozi bora katika ngazi zote.

Jokate anasisitiza pia wazazi kulea watoto katika maadili mazuri ili kupata viongozi bora kwani familia ni kiwanda cha kuzalisha viongozi bora pia. "Hatuwezi kuwa na viongozi bora bila kutengenezwa, viongozi bora wanatoka kwenye familia, wanatoka kwa wazazi na walezi, jukumu hilo haliwezi kukwepeka," amesema Jokate.

Aidha, nitoe rai kwa wazazi na walezi kuufanyia kazi ushauri huu wa Jokate, Katibu Mkuu wa UWT.

Ni ushauri uliokuja wakati sahihi ambao kama nchi, tupo katika kazi kubwa ya kujenga jamii yenye maadili mazuri kutokana na uwepo wa mmomonyoko wa maadili. Iwe ni kiu ya kila mzazi kuona watoto wake wanakuwa na tabia njema. Kama msingi na kiwanda cha malezi ambacho ni familia kikiyumba na kushindwa kutimiza majukumu yake ya kimalezi ipasavyo, mmomonyoko wa maadili utaendelea. Wazazi turudi katika nafasi zetu za kusimamia malezi ya watoto wetu, kwani bado tunayo nafasi ya kuokoa kiazi hiki na kijacho, hatujachelewa.

Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.

**Maoni: 0620 800 462.**

Kolamu



Hamisi Kibari

TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA

Simu: 0758143457

# Tujiulize kwa nini vijana sasa hawaaminiki kukabidhiwa biashara

PALE mtaani kwangu, kuna bucha mbili maarufu zinazouza nyama na samaki. Lakini hivi ninavyoongea, bucha moja imefungwa na nyingine iliyobaki, anayeuza sasa ni mtu mzima.

Nilipata kuzungumza na huyo mtu mzima kwa nini kijana aliyezoea kunihudumia simuoni.

Akaniambia alikaribia kufunga bucha ilipokuwa ikiendeshwa na huyo kijana kwa sababu ni hasara juu ya hasara alizokuwa akipata na visingizio kibao.

"Kabla ya huyo kijana nilishabadilisha hapa vijana wawili. Wanaanza kazi vizuri kisha wanaingia kwenye udokozi. Angalia sasa nimekaa mwenyewe, napata faida na ninatamani kufungua bucha nyingine mahala kwingine lakini kila nikifikiria hawa vijana wetu wa sasa wasivyo waaminifu, nasita kufungua," alisema huyo bwana.

Aliniambia kwamba kijana niliyemuulizia alikuwa akimlipa mshahara huku akiwa na uhakika wa kula mlo mzuri asubuhi na mchana, lakini kwa sasa anajuta.

"Kishakuja hapa mara kadhaa kuniomba msamaha arudi kazini, wala sitaki kusikia. Mbali na mshahara, nilimtengea pesa ya kifungua kinywa na chakula cha mchana hotelini. Alikuwa anakunywa chai nzuri na chakula kizuri wakati mwingine kuliko hata mimi na familia yangu nyumbani!

"Nimeamua kuacha shughuli yangu nyingine iliyokuwa inaniingizia pia kipato ili nikae hapa kwenye bucha. Naona manufaa," alisema.

Aliniambia katika utafiti wake amegundua kwamba vijana wengi wamewaangusha sana wafanyabiashara.

"Wafanyabiashara lukuki, hasa wa maduka, wameangushwa na uaminifu wa hovyo wa vijana. Baadhi yao ni watu ambao bado wako kwenye ajira, wamechukua mikopo ili kufungua biashara waongeze kipato kwa sababu maisha ni magumu lakini vijana wetu hawa wa leo wamewafilisi," alisema.

Kuna hii siku nyingine ambayo nilikutana na mama mmoja mstaafu, tena mjane na ambaye ametanguliza mbele ya haki watoto wake wote akanisimulia mkasa uliokaribia kunitoa machozi.

Yeye alipostaafu, alianza na vijana ambao ni wanandugu na kuwekeza kwenye biashara ya mashamba ya miti ya mbao lakini wakawa wanauza mbao nzuri bila yeye kujua, yeye wakimletea mbao zisizofaa (rejects) na kuishia kupata hasara.

Akasema amefanya biashara kadhaa zikiwemo za maduka lakini akawa anaangushwa na vijana anaowaamini.

Akasema biashara yake ya karibuni baada ya kuuza mali zake ili kupata mtaji, ilikuwa ni mgahawa wa kisasa uliojikita katika kuuza chips na bugger, yaani vyakula vya haraka, vya kuondoka navyo.

"Unajua mimi ni mzee, siwezi kukaa pale kwenye mgahawa muda wote. Halafu niseme tu kwamba sisi ambao tumezoea kukaa ofisini miaka na miaka ni wazito kukaa kwenye biashara lakini hawa vijana tunaowaweka si waaminifu kabisa."

Huyo mjane aliniambia kwamba vijana aliowaamini na kuwapa mradi huo, nao pia walifungua kijiwe chao maeneo hayo hayo, lakini Mungu si Athumani, kijiwe chao hakikumaliza miezi mitatu kikasambaratika!

Wakati mimi ninaamini bado kuna vijana waaminifu japo kwa asilimia chache lakini mjane huyo ambaye sasa ameanza kuishi kwa kutegemea ndugu anaamini kwamba waaminifu sasa hivi hakuna.

"Sasa hivi ni kama waaminifu hakuna. Si vijana tu bali hata watu wazima. Ajabu tatizo la uaminifu lipo hadi kwa viongozi wa dini. Yaani hizi ni dalili za mwisho wa dunia," alisema.

Juzi, nilienda saluni kunyoa, nikakuta kinyozi mpya'. Nilipouliza niliyemzoea nikakutana na majibu kama ya kwenye bucha. Niliyemuuliza kumbe ndiye mmiliki wa saluni!

"Nimemtimua, ndiyo maana nimeamua kukaa mwenyewe. Nimekaa wiki tatu tu hapa, tena kipindi hiki cha mgawo wa umeme lakini nimeshafanya mabadiliko. Kama unavyoona tayari nimenunua TV," aliniambia mmiliki huyo ambaye bado kijana pia.

Akaniambia kwamba tangu amefungua saluni hiyo huku yeye akinyoa katika saluni yake nyingine ambayo sasa ameweka mtu mwingine kwa matazamio, huyu niliyekuwa namuulizia ni kijana wa tatu kumtimua!

"Yaani hapa nilikuwa sipati pesa. Kila siku ni hadithi tu lakini nimekaa mwenyewe pesa ninapata na mgawo wa umeme

> **Sasa hivi ni kama waaminifu hakuna. Si vijana tu bali hata watu wazima. Ajabu tatizo la uaminifu lipo hadi kwa viongozi wa dini. Yaani hizi ni dalili za mwisho wa dunia.**

ukiisha nitaleta kinyozi mwingine tusaidiane ili wateja wasikae sana foleni," akasema.

Akaongeza, "kuna mmoja amekaa hapa muda mrefu sana na ndiye 'amenipiga' pesa kwa muda mrefu pia lakini ameshindwa hata kuanzisha saluni yake. Heri hata angeanzisha saluni ingemsaidia lakini nasikia pesa yote alikuwa anahonga wanawake tu. Wanashindana kuja hapa saluni kuchukua matumizi."

Nimejiuliza hii hali ya vijana wa siku hizi kufanya kile ambacho mimi ninakiona kama 'kula mtaji' kwa maana ya kutokuwa waaminifu kiasi cha kufilisi mahala panapowahakikishia kipato, kinatokana na nini?

Ninasema vijana wa siku hizi kwa sababu baba yangu mzazi anasimulia kwamba aliwahi kufanya kazi kwa Wahindi, Kisumu nchini Kenya lakini kwa jinsi alivyokuwa mwaminifu, wakati anawaaga baada ya kuamua kurejea nyumbani walisikitika sana.

Hata baba yangu mdogo pia amekuwa akifanya kazi kwenye kampuni moja kubwa ya Wahindi pale Mwanza lakini ametokea kuwa mboni ya jicho lao.

Mlolongo wa kizazi cha wazee wangu ambao waliheshimu kazi za watu walizokabidhiwa, wakiziendesha kama za kwao binafsi, ni mrefu sana.

Pale Musoma, kwa mfano, kuna Mzee wangu mmoja maarufu akiitwa Jalala Soli (sasa marehemu) alikuwa fundi kwenye kampuni ya Musoma Bus Service ambayo wamiliki wake walikuwa Wahindi pia lakini alipostaafu, waliamua kumpa basi afanyie biashara kwa kuheshimu juhudi zake kazini na uaminifu!

Utaona nimezungumzia zaidi vijana wanaoajiriwa kwenye sekta binafsi na isiyo rasmi lakini hofu yangu ni kwamba kwa kuwa hawa vijana ni zao la jamii hii hii, hata wanaoajiriwa kwenye sekta ya umma, mtazamo ni huu huu wa 'upigaji' kuliko matarajio ya mwajiri kwa maana ya serikali.

Swali ambalo nimekuwa ninajiuliza ni nini kinawasumbua vijana wengi wa siku hizi kukosa uadilifu? Nahisi ni tamaa, kuendekeza zinaa hasa kwa vijana wa kiume, malezi mabaya na kukosa hofu ya Mungu.

Vijana leo wanataka ndani ya muda mfupi awe kama fulani ambaye ameshajijenga kimaisha. Hali hii inampofusha kijana kushindwa kutunza na kuthamini mali ya mwajiri na maadili ya kazi. Anakuwa anawaza upigaji.

Tatizo pia liko katika kuendekeza wanawake kwa vijana wa kiume.

Lakini nadhani ipo shida pia katika malezi na ndio maana siku moja niliwahi kuandika nikihoji; 'Tatizo ni vijana wa siku hizi au malezi ya siku hizi?'. Nitarudia tena huo mjadala kama una maoni wasiliana nami kwa kunipigia au kwa ujumbe mfupi wa maandishi.

Lakini nimekuwa pia najiuliza kama tunawalea vijana wetu katika msingi ya kidini. Takribani kila dini inakataza wizi na dhuluma, kwani kumwibia tajiri ni kumdhulumu jasho lake na kutothamini uaminifu aliouweka kwako.

Sisi tunaoamini katika mafundisho ya dini, tunaamini pia kwamba fedha za kumwibia tajiri hazina baraka. Ni haramu, na ndio maana wengi hawaendelei kwazo. Utaona muda mfupi baada ya kutimuliwa huwa wanajuta na wale wanaofungua biashara zao kwa fedha za dhuluma huwa hawafiki mbali.

Dini ya Uislamu, kwa mfano, inafundisha kwamba dua ya mwenye kudhulumiwa haina pazia mbele ya Mwenyezi Mungu, hata kama anayeomba hana ukaribu na Mungu. Inapokelewa mara moja.

Yaani, hata kama unashinda kanisani au msikitini, wewe ni shekhe au mchungaji, ukimdhulumu mzinifu, mwongo, hasidi, mla rushwa au hata jambazi, dua yake dhidi yako inapokelewa na majibu unayapata hapa hapa duniani!

Nimeandika haya ili kuwataka vijana ambao ndio ninawelenga zaidi wajitathmini wanapoaminiwa wasifanye hiana. Wathamini mali za waajiri wao kama zao na mwisho wa siku watavuna baraka.

Nafundisho ya Uislamu yanaonesha pia kwamba kila mtu ni mchunga na siku ya kiyama ataulizwa na muumba wake kile alichokichunga. Wakati kiongozi wa umma hadi baba wa familia ataulizwa namna alivyofanya uadilifu kwa watu 'aliopewa' na Mungu kuwaongoza, sisi waajiriwa hadi mahausigeli tutaulizwa namna tulivyochunga mali za waajiri wetu.

Wazazi pia tuangalie namna tunavyowalea watoto wetu huku tukisisitiza dhana ya uaminifu kwani uzoefu unaonesha watu waaminifu hufaulu haraka katika maisha. Ni rahisi kukopesheka na kusaidiwa wanapokwama.

Kwa wanaofungua biashara nawasihi kuongeza umakini kwa vijana wanaowaajiri. Wahakikishe wanakuwa na wadhamini wa kuaminika ambao watabanwa na sheria kurejesha endapo vijana wanaokabidhiwa biashara wataiba, kufanya uzembe au kuhujumu.

Vyombo vya dola kuanzia ngazi ya mjumbe wa shina, serikali za mitaa hadi serikali kuu vinapofikishiwa malalamiko ya wafanyabiashara 'walioliziwa' na watu waliowaamini vitoe ushirikiano wa haraka.

Kwa vile nimegundua biashara nyingi zinakufa kutokana na hali hii, pengine vyombo vya kutunga sheria vinaweza kuja na sheria sasa zitakazosaidia kuwabana vijana wanaohujumu biashara hizi ndogondogo ili kuzilinda kwani kama tunatarajia zikue na kuwa kubwa lazima zilindwe.

Tunasikia baadhi ya wafanyabiashara wakubwa wa leo kama Bakhresa, Hayati Reginald Mengi na aliyewahi kuwa Rais wa Madagascar, Marc Ravalomanana, walianza biashara za kawaida, ndogo tu, lakini walipata wasimamizi waadilifu na leo biashara zao, mbali na kulipa kodi serikalini zinatoa ajira kwa mamilioni ya watu.

Vijana jitafakarini.

Siasa

# Tuwajenge na kuwaibua kina Dk Tulia wengi zaidi



Na Reubeni Lumbagala

NIANZE kwa kuuliza swali; Tunataka ushahidi gani juu ya uwezo wa wanawake katika uongozi?

Nimeamua kuanza na swali hili kutokana na dhana potofu ambayo ninaamini bado imo kwa baadhi ya watu kwamba wanawake hawana uwezo wa kumudu majukumu ya uongozi.

Dhana hii imepata nafasi na kuishi nayo kwenye baadhi ya mioyo ya watu wetu kutokana na historia ya jamii zilivyokuwa zikimchukulia mwanamke kwa muda mrefu.

Jamii nyingi duniani, si Tanzania pekee, kwa muda mrefu zimemchukulia mwanamke kama kiumbe dhaifu, asiyekuwa na uwezo wa kufanya yale ambayo wengi wamezoea kuona yakifanywa na wanaume na kwamba mahala pake ni jikoni au chumbani 'akimpumbaza' mumewe baada ya kazi na kulea watoto.

Lakini wataalamu wa mambo ya jinsi na jinsia wanatufundisha kwamba kunachomtofautisha mwanaume na mwanamke ni vitu takribani vitatu tu, basi.

Kwa upande wa mwanamke wataalamu wanasema asichoweza kufanya ni kitu kimoja tu, kwamba hawezi kutia mimba, basi, lakini taja vingine vyote utakavyotaja anaweza. Utake huo ndio ukweli na usitake ndio hivyohivyo!

Kwa upande wa mwanaume kuna vitu viwili tu ambavyo mwanamke anaweza lakini yeye mwanaume hawezi; kubeba mimba na kunyonyesha.

Ukija kwenye majukumu mengine ya kijinsia wote, mwanamke na mwanaume sawa kama nilivyokwisha dokeza. Kwa mfano, nani alikwambia mwanaume hawezi kupika wakati mkewe akitazama TV, kwamba mwanaume hawezi kufua nguo, kutandika kitanda na shughuli nyingine ambazo jamii yetu imejengwa kuamini kwamba ni kazi za kike?

Toka umezaliwa, ni mwanaume gani uliwahi kusikia kwa sababu ya kupika, kufua, kubeba mtoto au kudeki nyumba maumbile yake ya kiume, labda tuseme, ashakum si matusi, korodani zilitoweka? Hakuna.

Kwa hiyo kama ilivyo ukweli kwamba mwanamke anaweza kuchimba dhahabu, kubeba zege, kuendesha ndege, kuwa daktari wa meno au kazi yoyote utakayotaja ndivyo pia anavyoweza uongozi.

Kwa miongo mingi, dhana hii ya kumwona mtoto wa kike ni mtu wa kuolewa na shughuli zake ni jikoni imetuchelewesha sana kimaendeleo.

Kwa muda mrefu, hata haki ya kupata elimu, wasichana walinyimwa. Ungesikia mzazi akisema, "Mimi nisomeshe mtoto wa kike wa kazi gani?"

Kwa hiyo, kunyimwa haki ya kupata elimu kumeendelea kwa muda mrefu kuwarudisha nyuma kimaendeleo wasichana na wanawake.

Hata baadhi ya wanawake waliobahatika kusoma, kujiajiri au kuajiriwa, waume zao waliwakataza kufanya kazi ambayo ingemsaidia kuongeza kipato cha familia. Ujinga kweli kweli.

Alhamdulillah, kadri miaka ilivyokwenda, jamii zilianza kubadilika hata kama si kwa kasi sana. Taratibu wanawake ambao ndio wengi kwa idadi kuliko wanaume wakaanza kuaminika, wakapewa fursa ya kupata elimu na kufanya kazi ambazo awali iliaminika hawawezi kuzifanya.

Kwenye uongozi, wanawake pia walianza kuaminika kwa kuteuliwa na kuchaguliwa katika nafasi mbalimbali japo huku kwenye kuchaguliwa bado kuna kazi ya kufanya.

Kazi haijafanyika vya kutosha ili jamii kujitenga na 'mtazamo-dume" ndio maana bado bungeni tuna wabunge wengi wanaume wa kuchaguliwa kulinganisha na wanawake. Inatakiwa tufikie mahala tuachane na viti maalumu.

Pamoja na kwamba tupo kwenye karne ya ishirini na moja, yenye mabadiliko makubwa kuhusiana na uwezo wa wanawake,



wapo baadhi wa watu wanaishi kwenye karne ya ishirini na moja lakini wakiwa na mawazo ya karne ya kumi. Hili nalo ni tatizo kubwa ambalo hata makala yanalenga kulimaliza.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson ni miongoni mwa wanawake ambao ni chachu na darasa tosha la kubadili dhana dhana potofu kwa baadhi ya watu ndani na nje ya nchi yetu kuhusu uwezo wa wanawake katika uongozi.

Yeye alifanikiwa kuwa spika mwanamke wa pili katika Bunge letu la Tanzania, si kwa upendeleo wowote bali uwezo.

Hii imethibitisha uwezo mkubwa walionao wanawake kushika nafasi nyeti kama hiyo ya mhimili wa Bunge ambao una dhima ya kutunga sheria, kupitisha bajeti za serikali, kuihoji serikali na kuielekeza la kufanya kwa niaba yetu sisi wananchi.

Oktoba 27, 2023, Spika Dk. Tulia aliendelea kuwa darasa zuri la kuuthibitishia ulimwenguni juu ya uwezo wa wanawake katika uongozi kwa kushika nafasi nyeti duniani baada ya kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU).

Uchaguzi huo ulifanyika Luanda, nchini Angola ambapo Dk. Tulia alitangazwa mshindi kwa kupata kura 172 kati ya kura 303 zilizopigwa.

Wengine waliochuana na Dk Tulia ni pamoja na Adjidiarra Kanoute wa Senegeal aliyepata kura 59, Catherine Hara wa Malawi aliyepata kura 61 na Marwa Hagi wa Somalia aliyepata kura 11.

Kabla ya uchaguzi huo, Dk. Tulia alitaja vipaumbele vyake ikiwemo kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika bunge hilo na kuimarisha amani na ustawi wa IPU kimataifa.

Vilevile alisema atastawisha ushiriki wa makundi mbalimbali katika siasa kwenye Bunge la IPU, mathalani makundi ya wanawake, vijana na makundi mengine yasiyo na uwakilishi.

Katika kukazia sera zake, Dk. Tulia alisema "Mbali na vipaumbele nilivyovitaja, uongozi wangu utakwenda kutekeleza mikakati ya IPU ya 2022-2026 ya kujenga bunge imara na lenye nguvu, kukuza ushirikishwaji na uwakilishi ndani ya bunge."

Ushindi wa Dk. Tulia ni kielelezo muhimu kuwa wanawake wanaweza kumudu majukumu makubwa pengine kuzidi hata wanaume.

Kuaminiwa kwa daktari huyu wa falsafa za sheria kuongoza taasisi hii muhimu yenye maspika wa bunge 120 kutoka nchi mbalimbali duniani, kunazidi kuitangaza Tanzania kimataifa.

Pamoja na hilo, kunazidisha ujenzi wa mahusiano mazuri ya Tanzania na mataifa mengine ulimwengu na hivyo kuchagiza mafanikio ya mipango na mikakati ya kimaendeleo tuliyonayo inayohitaji ushirikiano na mataifa mengine ulimwenguni.

Rais Samia Suluhu Hassan ambaye pia ni mwanamke anayezidi kudhihirisha uwezo mkubwa wa uongozi walio nao wanawake aliompongeza Spika Tulia kwa kuchaguliwa kuwa Rais IPU.

"Kuchaguliwa kwako pia ni matokeo ya miaka mingi ya kazi, weledi na kujituma katika utumishi wa umma, mfano bora kwa watoto wa kike katika nchi yetu, Afrika na hata nje ya mipaka ya bara letu," amesema Rais Samia.

Watanzania tubadilike sasa. Tuamini wanawake wanaweza kumudu majukumu ya uongozi.

Lakini ni muhimu kuweka angalizo kwa wasichana na wanawake kufahamu kuwa hawatakubalika na kuaminika kwenye nafasi za uongozi kwa kwa sababu ya jinsi zao pekee, bali kwa uwezo, maarifa, uzoefu, uadilifu na uzalendo walionao katika nchi na kazi.

Dk. Tulia anaingia kwenye historia kubwa ulimwenguni ambapo anakuwa mwanamke wa kwanza kuongoza bunge hilo lenye nchi wanachama 179 na wabunge 705 wanaoziwakilisha nchi zao.

Ni kwa mantiki niungane na wengine kukupongeza kwa dhati kabisa Dk. Tulia kwa kuaminiwa katika nafasi hiyo. Mungu akutangulie, akusaidie na kukuwezesha kwenye majukumu mapya.

Shime wazazi na taifa kwa ujumla tuendelee kuwajenga na kuwaibua akina Dk. Tulia wengi zaidi.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma. Mawasiliano yake ni 0620 800 462.***





Jamii

# Tukatae ukeketaji



**Na Reubeni Lumbagala**

Ukatili dhidi ya kiumbehai chochote iwe ni binadamu, mnyama au ndege haukubaliki hata kidogo.

Viumbehai vimeumbwa na Mwenyezi Mungu vifurahie maisha na kufurahia uumbaji wa Mungu hapa duniani na hivyo wanyama wana haki zao za msingi. Hata ukifuga mbuzi, kabla ya kumchinja kwa ajili ya kitoweo, hauruhusiwi kumnyanyasa.

Yapo mafundisho katika baadhi ya madhehebu ya dini yanayoonesha kwamba kuna mwanamke alifunuliwa akihukumiwa na Mwenyezi Mungu kwenda motoni kutokana na kumtesa paka na mwingine kwenda mbinguni kwa kumwokoa mbwa na kiu kali.

Binadamu kama kiumbehai mwenye akili, utashi, uwezo mkubwa wa kufikiri na aliyepewa mamlaka na Mungu ya kutawala viumbe vingine anapaswa kuwa mfano wa kuigwa katika kuhakikisha dunia inakuwa sehemu nzuri na salama kwa ajili ya kuishi.

Moja ya changamoto inayoikabili dunia kwa sasa ni ukatili hasa wa kijinsia.

Ukatili huu umekuwa ukifanywa na binadamu dhidi ya binadamu mwenzake. Ni ukatili unaohusisha ubakaji, ukeketaji, ndoa za utotoni, mauaji na vipigo.

Kutokana na ongezeko la vitendo vya kikatili duniani na hasa katika nchi zinazoendelea, juhudi mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa kitaifa na kimataifa.

Malengo ni kuhakikisha kunakuwepo na mijadala mbalimbali ili kuja na maazimio ya pamoja na namna bora ya kumaliza vitendo vya kikatili ambavyo ni adui wa kufanikisha mipango mingi ya maendeleo.

Tanzania imepata heshima ya kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Pili wa Kimataifa wa Kutokomeza Ukeketeji ulio chini ya nchi wanachama wa Umoja wa Afrika (AU). Ni kwa mantiki hiyo, makala haya yatajikita kwenye eneo hilo la ukeketaji na hizo aina nyingine za ukatili wa kijinsia tutazingumzia siku nyingine panapo majaaliwa.

Kabla ya kwenda kwenye mkutano, tuangalie maana ya ukeketaji. Kwa mujibu wa wikipedia, ukeketaji (pia: huitwa tohara ya mwanamke) ni tendo la kukata sehemu za nje za viungo vya uzazi vya mwanamke. Kwa lugha nyingine ni 'kuziharibu'.

Ukeketaji una madhara ya muda mfupi na ya muda mrefu. Madhara ya muda mfupi ni kifo kutokana na kutokwa damu nyingi na maumivu makali, uharibifu mkubwa wa mfumo wa nje wa viungo vya uzazi pamoja na hatari ya kupata maambukizi.

Madhara ya muda mrefu ni pamoja na maumivu makali ya muda mrefu maambukizi – ikiwemo maambukizi ya mara kwa mara ya njia ya mkojo na kupungua kwa raha ya kujamiiana.

Lakini pia kuna madhara ya kisaikolojia, kama vile msongo wa mawazo utokanao na maumivu, kuongezeka kwa hatari za kujifungua kwa njia ya upasuaji, kuongezeka kwa vifo vya uzazi na kuongezeka kwa hatari za vifo vya watoto wachanga.

Madhara mengine ya muda mrefu ni kuongezeka kwa hatari ya watoto kuzaliwa kabla ya muda, kutoka damu nyingi wakati na baada ya kujifungua, watoto kuzaliwa na uzito mdogo (njiti) na uwepo wa madhara zaidi kwenye njia ya mkojo kwa wagonjwa wenye fistula ambao walifanyiwa ukeketaji.

Utafiti uliofanywa Tarime mwaka 2012 ulionesha kwamba ujio wa mgodi wa North Mara uliosababisha kuja pia kwa wanawake wengi wakiwemo wafanyabiashara katika wilaya hiyo ulihatarisha ndoa nyingi sana.

> **Ukeketaji unaondoa utu wa mtoto wa kike na wanawake, kila msichana anaweza kukua bila kivuli cha ukeketaji, hatuwezi kufikia dira ya maendeleo ya Tanzania 2030 ikiwa mamilioni ya wasichana wataendelea kukeketwa. Lazima tuseme inatosha ili kulinda wanawake milioni 68 walio katika hatari ya kukeketwa.**

Kisa? Wanaume wakikutana na wanawake wasiokeketwa 'huinjoi' zaidi tendo la ndoa na kuwatelekeza wake zao waliokeketwa!

Utafiti ulionesha pia matatizo ya kijamii na kisaikolojia kwamba wasichana waliokeketwa wakisafiri nje ya wilaya zao walikuwa wanaogopa 'kudeti' na wanaume wanaotoka katika jamii zisizokeketa wakihofia aibu ya maumbile yao yaliyoharibiwa!

Pia wale waliojifungulia katika mikoa isiyokeketa, walieleza kupewa maneno makali na hata kutukanwa na wauguzi na hivyo wengine kuogopa kwenda kujifungulia hospitalini.

Ingawa asili ya ukeketaji ni dhana ya kuwapunguzia wanawake mihemuko ya kimapenzi ili wawe waaminifu katika ndoa, lakini jamii zinazokeketa zimekuwa zikidanganya wanajamii kupitia imani zisizo za kisayansi ili kudumisha mila hiyo dhalili.

Madai ya wazee wa mila katika jamii zinazokeketa ni uongo kwamba mwanamke asiyekeketwa huleta mikosi katika familia na jamii kwa ujumla.

Kwa jamii ya Wakurya, kwa mfano, kifo kikitokea kwenye familia au mvua kwenye kijiji zikachelewa kunyesha, mwanamke au wanawake wasiokeketwa, kule wanaitwa 'wasaghane' ndio hunyooshewa kidole.

Mkutano dhidi ya ukeketaji umefanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere Dar es Salaam kuanzia Oktoba 9 hadi 11, 2023 huku zaidi ya washiriki 900 wakihudhuria mkutano huo.

Miongoni mwa washiriki hao, 200 ni washiriki wa ndani kwa maana ya Watanzania na 700 ni kutoka mataifa mengine

Ajenda kubwa ni kuunganisha nguvu ya pamoja dhidi vitendo vya ukeketaji.

Mkutano huu unachagizwa na kaulimbiu isemayo "Mabadiliko katika kizazi kimoja kwenda kingine ni muhimu katika kutokomeza vitendo vya ukeketaji" (*Changes in a Generation*).

Aidha, katika mkutano huo, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima alisema takwimu zinaonyesha kuwa wanawake na watoto wa kike milioni 200 ulimwenguni kote wamekeketwa.

Alisema miongoni mwao, milioni 20 wamefanyiwa dhuluma hiyo na wataalamu wa afya na kwamba watoto wa kike zaidi ya milioni 60 wapo katika hatari ya kukeketwa.

Hakika, hizi ni takwimu za kutisha za vitendo vya ukeketaji. Pia, ni jambo la kushangaza kuona wataalamu wa afya wakishiriki vitendo vya ukeketaji ambapo kwa taaluma yao walipaswa kujiepusha na vitendo hivyo kutokana na kuwa na uelewa mkubwa wa athari za ukeketaji.

Katika Mkutano huo, Waziri Gwajima alisema, "Ukeketaji unaondoa utu wa mtoto wa kike na wanawake, kila msichana anaweza kukua bila kivuli cha ukeketaji, hatuwezi kufikia dira ya maendeleo ya Tanzania 2030 ikiwa mamilioni ya wasichana wataendelea kukeketwa. Lazima tuseme inatosha ili kulinda wanawake milioni 68 walio katika hatari ya kukeketwa."

Takwimu za Umoja wa Mataifa za mwaka 2022, zinaonesha wasichana wenye umri wa miaka 15 hadi 49 wamekeketwa na asilimia 35 wamekeketwa wakiwa hawajafikia umri wa mwaka mmoja.

Takwimu hizo pia zinaonesha kwamba katika wanawake 10 mmoja amekeketwa.

Takwimu hizi ni wito kwa kila mwanajamii kushiriki kikamilifu katika mapambano ya kutokomeza ukeketaji na ukatili dhidi ya watoto wa kike ili wasichana na wanawake wajengewe mustakabali mwema wa maisha yao.

Pamoja na uwepo wa vitendo vya ukeketaji nchini lakini ni jambo la faraja ni kuona Tanzania imepiga hatua kubwa katika mapambano dhidi ya ukeketaji.

Kwa mujibu wa Kamishna wa Afya, Haki za Binadamu na Maendeleo ya Jamii (HHS) wa Umoja wa Afrika, Balozi Minate Samate, Tanzania imefanikiwa kupunguza ukeketaji kwa asilimia 75 huku ikiwa miongoni mwa nchi zenye viwango vya chini vya ukeketaji. Tanzania ina asilimia 15.

Pamoja na mafanikio haya, kama nchi hatupaswi kubweteka kwani ni wakati wa kutokomeza kabisa ukeketaji na kufikisha asilimia sifuri.

Kuendeleza ukeketaji ni kurudisha nyuma juhudi kubwa zinazofanywa na serikali pamoja na wadau wengine wa maendeleo za kumkomboa mwanamke kijamii na kiuchumi.

Takwimu zilizopo zinaonyesha ukeketaji katika mikoa ya Manyara ni asilimia 58, Dodoma asilimia 47, Arusha asilimia 42, Mara asilimia 32, Singida asilimia 31 na Tanga asilimia 14.

Jamii katika mikoa hii vinara wa ukeketaji inapaswa kubadilika kwani mila hii potofu imepitwa na wakati. Watanzania wanapaswa kuachana nayo kabisa kutokana na kuwa na athari nyingi kama ambazo tumezitaja hapo awali.

Wanaume kwa upande wao wanayo nafasi kubwa ya kufanikisha mapambano ya ukeketaji kwani kama wanaume watakataa kuoa wanawake waliokeketwa, ni dhahiri wazazi wakatakaa kukeketa watoto wao wa kike.

Mkondo wa sheria pia uwanase ngariba wote wanaoendekeza mila hii na ikiwezekana wasaidiwe mitaji wafanye biashara nyingine kwa kuwa wengi wanapokeketa ni mavuno.

Kuendeleza utamaduni wa kukeketa watoto wa kike ili waolewe, ni kuchochea ukeketaji na kurudisha nyuma maendeleo. Jamii tubadilike, tukatae ukeketaji na ukatili wa kijinsia kwa vitendo.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Mlali Sekondari ya wilayani Kongwa mkoa wa Dodoma. Mawasiliano yake ni 0620 800 462.***

Afya

# Mbinu za kutunza afya bora wakati wa ujauzito

**Na Godfrey Sanga kwa Msaada wa Mitandao**

KIPINDI cha ujauzito au kubeba mimba, kinaweza kuwa cha kufurahisha, lakini chenye msongo mkubwa wa mambo mengi ikiwemo mawazo.

Moja ya mambo ya kufurahisha ni wakati mama anajaribu kujua jinsi ya kuongea na mtoto tumboni.

Wakati unajiandaa kumleta (kumkaribisha) mtu mpya duniani, mwili wako utapitia mabadiliko makubwa, yanayoonekana na yasiyoonekana. Dalili za ujauzito hutofautiana kwa kiasi fulani baina ya watu pia.

Hivyo basi, inaeleweka kwamba utakuwa na maswali kuhusu ujauzito wako na namna ya kukufanya wewe na mtoto wako kuendelea kuwa salama na wenye afya.

**JE, UNAWEZAJE KUITUNZA AFYA BORA WAKATI WA UJAUZITO?**

Mama na mtoto wake, wanaweza kuendelea kuwa na afya bora kwa kupata chakula cha kutosha chenye virutubishi, kupumzika sana kila siku, kuepuka kemikali, pombe, moshi na sehemu kubwa ya dawa, kupata huduma kutoka kwa mkunga au mfanyakazi wa afya mwingine ambaye anaweza kutibu au kusaidia kupata matibabu kwa ajili ya tatizo lolote la kiafya ambalo linaweza kujitokeza na upendo pamoja na huruma.

**I. KULA VYAKULA VYENYE VIRUTUBISHO**

Mchanganyiko wa chakula chenye virutubishi kitamfanya mwanamke awe na nguvu na afya pia ili apate nguvu za kujifungua na kumhudumia mtoto.

Kumbuka mwanamke analazimika kula chakula cha kumtosha yeye na mwanawe. Hivyo anahitaji kula chakula zaidi kuliko watu wazima.

**II. ZUIA UPUNGUFU WA CHEMBE NYEKUNDU ZA DAMU (ANEMIA)**

Anemia (upungufu wa chembe nyekundu kwenye damu), hutokea sana wakati wa ujauzito, husababisha kujisikia mchovu kila mara.

Anemia ni hatari zaidi hasa kwa wajawazito kwa sababu damu hupotea wakati wa kujifungua.

Hii inaweza kuzidisha upungufu huo na kusababisha mama kupoteza maisha.

Zuia anemia kwa kula vyakula vyenye protini na wingi wa madini chuma na pia kutumia dawa ya kuongeza madini chuma mwilini.

**III. ASIDI YA FOLIKI**

Ukosefu wa asidi ya foliki (au vitamini ya foleti), kunaweza kusababisha hitilafu katika umbaaji wa mtoto na hata ulemavu.

Chagua dawa za kuongeza madini chuma mwilini ambazo zinajumuisha asidi ya foliki au dawa za kuongeza foliki mwilini.

**IV. VITAMINI A**

Mbogamboga za kijani na matunda ya rangi ya chungwa, zina vitamini A, kirutubishi ambacho kinahitajika kwa ajili ya afya ya macho.

Mjamzito anahitaji mbogamboga za kijani na matunda ya rangi ya chungwa zaidi kwa sababu vitamini A anayokula, hutumika kwanza kukidhi mahitaji ya mtoto. Ukosefu wa vitamini A, unaweza kusababisha kutoona usiku au upofu kwa ujumla.

**V. KUMPUMZIKA**

Ni muhimu mjamzito kusaidiwa majukumu ya kazi ili awe na muda mwingi wa kupumzika. Mkumbushe, hasa ujauzito unapozidi kukua, kupumzika na kuinua miguu yake juu mara kadhaa kwa siku au kulala chini wakati wa alfajiri.

**VI. EPUKA MATUMIZI YA BIDHAA HATARI**

Sigara na tumbaku hutajwa kuathiri mapafu ya mama na vinaweza kusabisha saratani na hata kifo. Moshi unaweza kusababisha mtoto kuzaliwa kabla ya muda wake au akiwa na uzito mdogo au akiwa amekwisha kufa.

**Pombe na dawa za kulevya**

Mjamzito anapokunywa pombe, inaweza kusababisha hitilafu za kudumu kwenye ubongo wa mtoto na mwili wake. Kadiri anavyozidi kunywa pombe nyingi, ndivyo madhara kwa mtoto yanavyoongezeka.

**Dawa za kawaida**

Dawa nyingi anapozitumia mwajamzito, pia humfikia mtoto wake. Kwa sababu watoto tumboni wanakuwa wadogo sana na wakiendelea kuumbika, dawa ambazo ni salama kwa mtu mzima zinaweza kusababisha hitilafu wakati wa kujifungua na hata madhara kwa mtoto. Hivyo wajawazito wanapaswa kuepuka kutumia dawa holela.

Lakini kuna baadhi ya magonjwa ni hatari sana kuyaachia bila kuyatibu katika kipindi chote cha ujauzito kama vile malaria, VVU, Ukimwi na maambukizi ya njia ya mkojo (U.T.I.)

Ili kujua iwapo dawa yoyote ile ni salama kutumia wakati wa ujauzito na wakati wa unyonyeshaji, muulize mfanyakazi wa afya mwenye uzoefu. Angalia pia sehemu ya dawa mwishoni mwa sura hi au rejea miongozo mingine juu ya matumizi ya dawa.

Kwa dawa ambazo zinahitajika, lakini siyo salama, kawaida huwa kuna dawa nyingine mbadala ambayo inaweza kutumika.

Dawa za asili na mimea/mitidawa, zinaweza kusababisha madhara zaidi kuliko kutoa tiba. Kitabu kiitwacho Dawa, vipimo na matibabu (kinaandaliwa) kimependekeza njia za kuzingatia unapotaka kufanya maamuzi juu ya matumizi ya dawa za asili.

**VII. EPUKA KUKUTANA NA WAGONJWA.**

Kuugua wakati wa Ujauzito, ni taabu kubwa. Ugonjwa unaweza kusababisha taabu kubwa katika kula na kutokula chakula cha kutosha humunyima mjamzito nguvu.

Epuka kukutana na wagonjwa kupunguza uwezekano wa kuambukizwa.

**VIII. KUTANA NA MKUNGA AU MHUDUMU WA AFYA**

Mkunga mzoefu au mfanyakazi wa afya mwingine anaweza kumshauri mwanamke mjamzito jinsi ya kuishi na afya nzuri na salama, kutibu magonjwa yote ya kawaida na kupunguza kero, na kutambua lini mwanamke mjamzito anapohitaji kutafuta msaada kwenye hospitali au kituo cha afya.

**IX. CHANJO**

Mwanamke mjamzito anapaswa kuchanjwa dhidi ya pepopunda (tetenasi) mapema iwezekanavyo katika ujauzito. Anatakiwa kupewa chanjo nyingine wiki 4 baadaye iwapo atakuwa hajapata chanjo zote. Hii husaidia kuwalinda wote wawili(mama na mtoto).

**X. VIPIMO VYA MAABARA**

Vipimo rahisi vinaweza kugundua baadhi ya magonjwa mengi ambayo ni hatari kwa wanawake na watoto wachanga. Vipimo hivi huwatahadharisha mama na mfanyakazi wa afya kuanza matibabu mara moja, hatua ambayo inaweza kuzuia matatizo makubwa wakati na baada ya kujifungua.

Kipimo cha VVU kinatakiwa kutolewa kwa akina mama wote wajawazito. Mwanamke anapogundua ana VVU, anaweza kuanza kutumia dawa ya kumsaidia afya yake na kumlinda mtoto asiambukizwe VVU.



Uchumi

# Sheria za kodi Tanzania

Na Sylivester K. Sebastian

Huu ni mwendelezo wa uchambuzi wa kina wa aina mbali mbali za kodi zinazotozwa kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kama ilivyoelezwa katika makala zilizopita, ufahamu wa sheria za kodi unarahisisha uanzishaji na uendeshaji wa shughuli za kiuchumi.

Aidha, uelewa mpana wa sheria hizi upekelekea utii wa sheria, upungufu wa migogoro ya kikodi na uleta ustawi wa jamii na ukuaji wa uchumi.

Makala zilizotangulia zilichambua aina i mbali mbali za kodi ikiwemo kodi ya mapato inayotakiwa kulipwa na mtu binafsi (mkazi au asiyemkazi).

Kodi ya mapato yatokanayo na ajirani kodi ambayo mtu yeyote mwenye ajira analazimika kuilipa serikalini kutokana na mapato yatokanayo na ajira yake.

Kodi hii hailipwi moja kwa moja na mwajiriwa kama kodi ya zuio (withholding tax).

Sheria ya kodi ya mapato Tanzania inatambua ajira kama shughuli ya aina yoyote (halali) afanyayo mtu kutokana na mkataba wa maandishi au wa mdomo. Mkataba huo unaweza kuwa wa kudumu au wa muda. Kwa mujibu wa sheria ya mapato Kibarua utambulika kama mwajiriwa.

Kipato cha mtu binafsi kitokanacho na ajira ni kipato au faida aipatayo mwajiriwa kutoka kwenye ajira yake ndani ya kipindi cha mwaka wa fedha husika.

Kifungu cha 7 cha Sheria ya Mapato Sura Na. 322 kimebainisha aina za malipo anayopokea mwajiriwa ambayo ulazimika kukatwa kodi ya mapato kwa upande mmoja na aina ya malipo ambayo hayakatwi kodi kwa upande mwigine.

Mapato ya mwezi yanayokatwa kodi ni pamoja na mshahara, malipo kwa kazi za ziada, bonasi, kamisheni, na marupurupu mengine, yatokanayo na ajira.

Kifungu cha 81 cha Sheria ya Kodi ya Mapato kinamtaka mwajiri kushikilia kodi kutoka kwa malipo aliyolipwa mfanyakazi kwa kiwango kilichowekwa kwa mujibu wa sheria.

Mwajiri anahitajika kwa mujibu wa kifungu cha 84(1) kulipia kodi aliyozuia kwa TRA ndani ya siku saba (7) baada ya mwisho wa kila mwezi.

Mwajiri analojukumu la kukusanya kodi hii kutoka kwa waajiriwa alionao bila ya kujari kama waajiriwa hao wameajiriwa na mwajiri mwingine kwa wakati huo.

Viwango vya kodi ambavyo mtu anatakiwa kukatwa kwa mujibu wa sheria ya kodi ya mapato, hutofautiana kulingana na kiwango cha kipato anachopata mtu kwa mwezi. Viwango hivi vimekuwa vikibadilika mara kwa mara kutokana na jitihada za serikali kupunguza viwango hivyo ili kupunguza ukali wa maisha kwa wafanyakazi.

Kwa mwaka huu (2023) viwango vya makato ya kodi kwa wafanyakazi Tanzania ni kama ifuatavyo;

- Mfanyakazi anayepokea mshahara chini ya Sh.270,000 hakatwi kodi.
- Mfanyakazi anayepokea mshahara kuanzia Sh.270,000 hadi Sh.520,000 hukatwa kodi ya asilimia nane (8%) ya kiasi kinachozidi baada ya Sh.270,000.
- Wafanyakazi wanaolipwa kiasi cha kuanzia Sh. 520,000 hadi Sh.760,000 hulipa kodi ya Sh.20,000 ukiongezea na asilimia ishirini (20%) kwa kiasi kinachozidi Sh.520,000.
- Vile vile kwa wafanyakazi wanaopokea mshahara kuanzia Sh.760,000 hadi Sh. 1,000,000hulipa kodi ya mapato kiasi cha Sh. 68,000 ukiongeza asilimi ishirini na tano (25%)ya kiasi kinachozidi Sh. 760,000.
- Wafanyakazi wanaolipwa mshahara kanzia Sh. 1,000,000 wanatakiwa kulipa kodi kiasi cha Sh.128,000 ukiongeza asilimia thelathini (30%) ya kiasi kinachozidi Sh. 1,000,000.
- Kwa wafanyakazi wasio wakazi walio ajiriwa na mwajiri mkazi, mapato yao hutozwa kodi ya zuio ya asilimia kumi na tano (15%) tu.
- Wafanyakazi wakazi na wasiowakazi wenye ajira ya ziada watakatwa Kodi ya zuio itokanayo na ajira ya ziada kiwango cha asilimia thelathini (30%.)

## MSAMAHA WA KODI KWA WATUMISHI WA UMMA

Msamaha wa kodi ni punguzo, nafuu au kuondolewa kabisa kwa wajibu wa kisheria wa kulipa kodi au tozo mbalimbali kwa Serikali. Msamaha wa kodi kwa watumishi wa umma utolewa na serikali kwa waheshimiwa wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzaniana na watumishi wa umma. Msamaha huu hutolewa kwa ajili ya kununua gari moja kwa kipindi cha miaka minne.

***Mtumishi wa umma ni nani?***

Kwa mujibu wa sheria, mtumishi wa umma ni mwajiriwa anayehudumu katika ajira ya kudumu katika taasisi zifuatavyo;

- erikali Kuu;
- Serikali za mitaa;
- Shirikia la serikali (ambalo bajeti yake inagaramiwa na Serikari kwa 50%-Mfano Tanesco)
- Taasisi za Serikali. Mfano NECTA n.k.

Msingi wa kisheria wa utoaji wa msamaha huu hutokana na matangazo ya serikali (GN) kama ifuatavyo;

- Ushuru wa Forodha (Customs Import Duty) Tangazo la Serikali Na. 520 (GN. 520)
- Ushuru wa Bidhaa (Customs Excise Duty) Tangazo la Serikali Na. 522(GN. 522)

N.B: Pamoja na kwamba tunaita ni msamaha, maana halisi siyo msamaha bali ni msaada wa kulipiwa na Serikali. Hili hufanyika kwa njia ya Vocha ya Hazina (Treasury Voucher System) ambapo Serikali huwa na fungu la fedha maalumu kwa kazi hii.

## VIGEZO VYAMAGARI YENYE MSAMAHA WA KODI

- Magari aina ya 'Saloon'
- Station wagon
- Pick up ambazo zinabeba mzigo chini ya tani 2
- Gari ambazo uwezo wa kubeba abiria hauzidi siti 9
- Gari isizidi umri wa miaka 10 tangu lilipotengenezwa
- Gari lenye umri wa miaka 0 hadi 7 litapata msamaha bila kodi ya uchakavu.
- Gari ambazo ujazo wake wa injini hauzidi cc 3000 (hata hivyo, kwa waheshimiwa wabunge (cc) haina ukomo)

## UTARATIBU WA KUOMBA MSAMAHA

Baada ya kuagiza gari na kupokea nyaraka za manunuzi mnufaika wa msamaha atafanya yafuatayo;

- Kujaza fomu za maombi ya msamaha nakala (4) zinazopatikana katika tovuti ya Mamlaka ya Mapato ambapo Sehemu A itajazwa na muombaji na sehemu B. ya fomu itajazwa na mwajiri.
- Nyaraka za ununuzi wa gari, nyaraka za kiforodha na nyaraka muhimu za kiutumishi ili kuthibitisha utumishi wake.
- Kuandika barua ya maombi ya msamaha kwenda kwa Afisa Masuuli wake.
- Mwombaji lazima awe na TIN
- Picha nne za passport size zinazotokana na negative moja
- Barua ya Utambulisho kutoka kwa muajiri (mtendaji mkuu taasisi anayofanyia kazi muombaji)
- Slip ya Mshahara ya karibuni
- Barua ya ajira na barua ya kupandishwa daraja ya karinuni
- Nakala ya kitambulisho cha kazi
- Ankara ya gari (Invoice)
- Muswada wa shehena (Bill of Lading) au Muswada wa Shehena wa Ndege (Air Waybill) au Muswada wa shehena inayoingia kwa njia ya barabara (Road Consignment Note)
- Cheti cha kusafirisha gari nje ya nchi toka nchi inakotoka na tafsiri yake kama gari inatoka Japan au UAE.
- Kadi au cheti cha kufuta usajili toka nchi inakotoka.
- kadi ya usajili toka nchi inakotoka.

Mtumishi anawajibika kurejesha fomu zilizojazwa Mamlaka ya Mapato Tanzania Idara ya Kodi za Forodha kwa ajili ya kukadiriwa kodi.

Mamlaka ya Mapato Tanzania itawasilisha hati ya madai Wizara ya Fedha inayoonesha kiasi kinachopaswa kulipwa na Serikali kama msamaha wa kodi kwa ajili ya mtumishi.

Aidha mtumishi atapaswa kulipia kiwango kinachompasa ambacho ni jumla ya kodi zote toa kiasi cha msamaha.

## MASHARTI YA MSAMAHA

- Msamaha hauhamishwi.
- Msamaha utakoma ikiwa mtumishi ataacha kuwa mtumishi ndani ya miaka 4 toka kutolewa kwake.
- Msamaha huu hautolewi kwa watumishi walio masomoni au anae fanya kazi ya muda nje ya nchi.
- Kabla ya kuuza, kuhamisha umiliki au kugawa gari iliyonufaika na msamaha huu ni sharti idhini iombwe kwa Kamishna wa Forodha
- Ni muhimu kutunza kumbukumbu za misamaha kwa sababu nyingi ikiwemo ukaguzi na kuandaa taarifa za matumizi.

## SABABU ZINAZOWEZA KUSABABISHA MAOMBI YA MSAMAHA HUU KUCHELEWA

- Maombi kutoelekezwa ofisi sahihi
- Maombi kukosa viambatishi hitajika, kwa mujibu wa sheria
- Maelezo ya maombi kutotolewa kwa ufasaha
- Kutofanya ufuatiliaji wa karibu




*itaendelea...*



Paul Mng'ong'o

## KLINIKI YA FIKRA

Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

# Unapita njia ipi kwenye maisha?

WENGI tumejengewa imani kuwa, maisha yanakuja yenyewe na ni kudra tu.

Tumeamini kuwa kila kinachotutokea, tumepangiwa au ni bahati. Dhana hii pamoja na kuwa ina ukweli, lakini imepokelewa na kutumika vibaya kwa jamii husussan za Ki-Afrika, wakidhani ndiyo majaliwa na hakuna namna nyingine.


Dhana hii imefanya watu kutopanga malengo na kuamua hatma zao. Jamii zilizoendelea walielewa kuwa, maisha yanapangwa na mhusika kuanzia kwenye aina ya taarifa (maarifa) anayoyapokea zaidi ambayo yanajenga mtazamo wake na kuathiri ukuaji wake.

Kila mtu ana uwezo ndani yake. Wewe unayesoma makala hii pia umezaliwa na uwezo mkubwa ndani yako, uwezo unaoweza kubadilisha maisha yako na ya wale wanaokuzunguka, uwezo unaoweza kuleta mabadiliko kwenye eneo lako la kazi, uwezo unaoweza kubadili hali yako ya kiuchumi na kimahusiano, huu ni ukweli ambao watu wengi hawaukubali au wanaukubali ila hawauamini. Lakini haitoshi tu kujua una uwezo ndani yako, unatakiwa uuendeleze huo uwezo ukitambua kuwa, ziko njia mbili ambazo wanapita watu wote.

Njia ya kwanza inaitwa “Njia kuelekea Ukuu” (the path to Greatness). Njia hii inakufanya wewe kuhusika kikamilifu kuibua na kutumia nguvu na uwezo ulionao. Mchakato huo ndiyo safari ya kuyabadili maisha yako na kutoa mchango wako kugusa na kuhudumia wengine. Njia hii hufuata mtiririko wa ukuaji unaoanzia ndani kuja nje Sequential growth - from inside-out). Mtiririko huu unaanza na wewe kuamua maeneo ambayo unataka kuwa bora, unachagua aina ya taarifa na maarifa yatakayokufikisha kwenye ubora unaoukusudia, tatu ni kujitoa kwa dhati kwa kupunguza mambo mengine ili kutoa muda wa kutosha kujipatia maarifa hayo mahsusi.

Mafanikio yote huanzia ndani yako, lakini kinachofanya ukuaji ndani yako ni aina ya taarifa na maarifa ambayo unayaruhusu kuingia ndani yako mara kwa mara. Njia hii ya kwanza inatengeneza nguvu ya ubunifu (Creative Forces) ndani yako kukuwezesha kuwajibika kufanya maamuzi ya kuzishinda changamoto zote zilizo ndani na nje yako. Kikubwa cha kufahamu ni kwamba, njia hii ni ile ambayo wewe unapanga na kuamua na kuweka bidii. Hii ndiyo yenye asilimia kubwa ya kufikisha kwenye ukuu.

Njia ya pili inaitwa Njia ya Kujifananisha (The path to Mediocrity).



Njia hii inauzima au kuua uwezo uliomo ndani yako, watu wengi bila ya kujua wanapita njia hii. Kwenye njia hii, uwezo na nguvu ndani yako hazihusiki kwenye ukuaji wako, unajikuta unaishi tu kulingana na mazingira yako, unaangalia tu wanaokuzungua wanafanyaje na hakuna chujio ndani yako. Lile eneo la maamuzi (Centre of decision and choices) ndani yako linakuwa halifanyi kazi. Kinachotokea ni kuathiriwa moja kwa moja na mambo ya nje nawe kuwa hivyohivyo mazingira ya nje yalivyo. Kwenye njia hii, maisha yanaamua na kukufanya kuwa mtu wa aina fulani (culture software) kwa maana ya kwamba, mfumo unaokutengeneza unakuwa nje ndani (outside-in),ambapo unajikuta unakuwa na mtindo

> **Lakini kumbuka haitoshi kuutambua na kuuendeleza tu uwezo wako, unahitaji kujua namna ya kuutumia huo uwezo (know how to express your...**

wa kutafuta tu njia rahisi kuishi (short-cut au quick fix kwenye maisha).

Ni vyema kama utaamua kuifuata njia ya kwanza (The path to Greatness) sababu itakayoendeleza na kukuza nguvu na uwezo wako, itakutengeneza na kukujengea uwezo wa kutoa mchango wako duniani.

Lakini kumbuka haitoshi kuutambua na kuuendeleza tu uwezo wako, unahitaji kujua namna ya kuutumia huo uwezo (know how to express your potential) katika namna ambayo itagusa maisha yako na maisha ya watu wengine.

Mwandishi Stephen Convey katika kitabu “The 8th habit” amefundisha vizuri njia hii ya “the Path to Greatness”, unaweza kutafuta kitabu chako ukasoma.

Kliniki ya Fikra inatambua na kumshukuru mchango mkubwa wa Mwalimu na Paul Masatu kwenye ujenzi wa makala hii. Yeye amejenga msingi wa maarifa haya leo. Mungu ambariki kwa mchango mkubwa.

Kama unapenda kupata ushauri au usimamizi wa karibu katika kuishi mwongozo huu au miongozo iliyotangulia, (Unaweza kuwa Taasisi Binafsi au ya Serikali, Kikundi cha kijamii, Kanisa, Umoja, NGO, Mtu binafsi n.k) karibu sana, tutashirikiana kwa neema na msaada wa Mungu.

Karibu tuwasiliane kwa namba 0676055444 au barua pepe mngongopaul@yahoo.com na kwenye mitandao ya kijamii.

Paul Mng'ong'o



Na Hamisi Kibari

Mtanzania wa kwanza kushinda Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu

# Niko tayari kwa kifo - 6

**Chris, anajikuta akinogewa na penzi la Joyce, Miss Tabora wa zamani. Mahusiano hayo yanamfanya ajifunze kunywa pombe na kutelekeza familia.**

**Mkewe anapoamua kwenda kwao kulalamika, Chris anahamia nyumbani kwake na hawara yake huyo Joyce ili kupunguza gharama za kuishi hoteli. Mkewe anaporejea ghafla akiwaacha nyuma wazazi wake kuja kusikiliza ugomvi usioisha, kunatokea mtafaruku wa mkewe na hawara. Chris anampiga mkewe hadi anazirai.**

**Nini kitatokea?**

ALIMWELEZA kilichotokea na kumtaka abaki na mtoto huyo wakati wanawahi hospitali, lakini Joyce alikataa.

"Siwezi kulala na toto la mtu," alisema Joyce akibetua midomo.

"Kuwa na huruma kidogo Joy, tunazidi kuchelewa. Huyu mwanamke anaweza kutufia hapa. Akifa hiyo ni kesi kubwa sana."

"Mpeleke kwa dada yako. Si kaka yake yuko huko. Mpeleke. Mama yake akifa mimi inanihusu nini?"

"Joy, unadhani ni rahisi kiasi hicho dada kunielewa?"

"Mtoto mwenyewe kalala. Ungemwacha akiwa amelala hadi asubuhi. Asingekuwa chochote lakini mimi sina muda wa kulala na toto la mtu," alisema Joyce.

Chris aliamua kwenda kumbembeleza mhudumu wa hoteli hiyo ya Lemon Tree kubaki na mwanae Huba. Mhudumu huyo alikataa akihoji sababu.

"Mama yake anaumwa sana tunamkimbiza hospitali,"alijibu.

"Si mmechukua chumba hapa, kwani asiende kulala na Miss Tabora wako?"

"Naye ana matatizo... Mimi nikitoka tu hospitali ninakuja kumchukua," alisema akichomoa noti ya Sh 10,000 na kumpatia.

"Si kunakaribia kucha. Utakuja saa ngapi?"

"Wakisha mpokea mgonjwa. Nadhani ndani ya nusu saa hadi saa nzima... Naomba msaada wako tumwahishe mgonjwa hospitali."

"Haya. Usikose kuja kumchukua ukirejea. Nikishtuka usingizini ninamleta chumbani kwenu."

"Wala usiwe na wasiwasi."

Kisha Chris alirudi haraka kwenye teksi. Akajaribu kumtikisa Mama Kenny, bado alikuwa hajitingishi.

Roho ilizidi kumwenda mbio akihofia kwamba anaweza akawa amemuua. Akamtaka dereva kuondoa gari haraka.

Wakiwa njiani, Chris alipata wazo la kumtelekeza Mama Kenny nje ya hospitali kwa kuwa iliaminika kwamba alikuwa kao kwa hiyo angeweza kudai mbele za watu kwamba hajui kilichompata kwa sababu hajamtia machoni.

Lakini akakumbuka kwamba alikuwa tayari ana mwanae Huba aliyemwacha kwa mhudumu. Angeelaza vipi kuhusu alivyompa mtoto huyo. Halafu akakumbuka mayowe ya Mama Kenny yalivyosababisha watu kuja pale mlangoni.

"Halafu kama Mama Kenny atarejewa na fahamu akasimulia yaliyotokea, nani ambaye atanielewa," akajisemea na kujishangaa kufikiria kitu cha hatari.

Kwa mara ya kwanza toka anogewe penzi la Joyce na kutaka kuwa naye kila wakati, alianza kuingiwa na imani kwa mkewe. Kwa mara ya kwanza alianza kuhisi iko shida kumbadilisha Joyce kumtii kama ilivyokuwa kwa Mama Kenny aliporejea majibu yake ya kukutaa kulala na Huba katika mazingira aliyokuwa anapitia.

Akawa anajiuliza maswali mengi pale atakapomuoa na kuachana kabisa na Mama Kenny.

"Yaani anasema Mama Kenny akifa yeye inamhusu nini, hajui hatari iliyopo kwangu.

Huyu mwanamke ananipenda kweli kama mimi ninavyompenda?" Akawa anajiuliza.

***

Chris alipomfikisha mkewe hospitali, alipolekwa mara moja chumba dharura na baada ya kuchunguzwa na daktari kwa muda baada ya Chris kudai alidondoka kwenye ngazi,

Mama Kenny ambaye daktari wa zamu alithibitisha kwamba bado yuko hai alihamishiwa chumba cha wagonjwa wenye kuhitaji uangalizi maalumu.

Chris alipumua sasa kusikia kauli ya daktari kwamba Mama Kenny bado hajafa lakini ana hali mbaya na inayotishia uhai wake.

Baadaye daktari aliyempokea wodi ya wagonjwa wanaihitaji uangalizi maalumu katika Hospitali ya Mkoa ya Kitete alimwita ofisini na kumtaka aketi kwenye kiti. Ilikuwa ni takribani saa nzima tangu wamfikishe hospitali na vipimo mbalimbali kuchukuliwa.

"Umesema unaitwa nani vile?" Alianza kumhoji daktari wa zamu wakati akisoma ripoti iliyoandikwa na daktari mwenzake wa chumba cha dharura." Naita Chrisostom Magati"

"Naangalia hii ripoti, umesema wewe ni mume wake huyu mgonjwa, siyo?"

"Eh... Ndiyo."

"Bwana Mzee, sema ukweli, siyo kwamba amepigwa?

Hata daktari mwenzangu nimeongea naye kwa simu anatilia shaka sababu za kumfanya mkeo apoteze fahamu," Akazidi kuhoji daktari. "Hapana... Ni kama nilivyosema dokta. Amepata ajali tu ya kuanguka kwenye ngazi. Kulitokea kutoelewana kidogo akawa ananikimbia." Daktari aliangalia saa yake. Ilikuwa ni saa tisa na ushei usiku."Bwana Mzee, usiku wote huu, alikuwa anafanya nini kwenye ngazi?"

"Mbona huniamini daktari?" Anajibu Chris baada ya kusita kwa sekunde kadhaa." Mr. Magati, usinidanganye. Huyu mwanamke kapigwa. Kuna kila dalili.

Haiwezekani mtu kuanguka kwenye ngazi halafu hali ikawa hivi.

> **Alimwacha mwanae akicheza kitandani, akaingia bafuni kujimwagia maji. Baada ya kuvaa nguo za kutokea siku hiyo alimchukua mwanae na kutoka naye sebuleni tayari kwenda kwa dada yake, Mwalimu Misango. Mpaka muda huo alikuwa hajajua atamweleza...**

Tena hujui hata kutunga uongo. Afadhali ungesema amepata ajali ya gari au bodaboda. Huyu tunapambana kuokoa uhai wake kwa sababu inaonesha amepata damage kwenye brain, hata kabla hajapimwa kwenye CT Scan kesho inaonekana ana severe brain injury. hatuwezi kumtibu mpaka suala hili lipitie polisi. Hii ni police case," alijibu daktari akiwa sasa amekunja uso.Chris alivuta pumzi na kuzishusha taratibu. Kisha akanyanyua uso wake:

Bwana daktari. Ukweli kulitokea kutoelewana kidogo baina yangu na huyu mama watoto wangu. Nimempiga baada ya kuja usiku huu akitokea kwa hawara. Alijua nimesafiri na mimi nilishaambiwa nikitoka naye anatoka... Imeniuma sana. Kwa kweli nilishikwa na hasira sana na nikajikuta nimempiga bila kutegemea.

Naomba msaada wako." Chris alishika mfukoni, akatoa Sh 100,000, akampa yule daktari ambaye alibaki akimtaza usoni wakati wote akijieleza bila kupepesa mcho.

"Naomba msaada wako, tafadhari". Daktari alisita kuchukua zile fedha, baadaye akachukua baada ya Chris kuamua kuongeza fedha kama hizo siku ya pili yake.

Akazichomeka kwenye mfuko wake wa shati bila kuhesabu.

"Unajua kuna mambo yanakutokea bila kutazamia. Kwa hiyo unakuwa hujajitayarisha. Naomba, wewe kama mwanaume mwenzangu unisaidie na kesho tutayamaliza. Nita Sikutegemea kabisa kama nitamuumiza kiasi hiki. Hii yote ni kwa sababu ya hasira," alizidi kusema Chris.

"Ninakuelewa Mr. Magati. Hayo ndio mambo ulipaswa kuniambia. Wanawake wanakera sana. Lakini hili ni gumu sana kumtibu bila ya kuwa na PF3."

"Ndio maana ninaomba unisaidie. Kumbuka shida haina mmoja na wala haina hodi. Leo yananikuta mimi, kesho yanaweza kukukuta wewe na mimi nikakusaidia ama mwanaume mwingine mwenzako. Wanaume ni kusaidiana."

"Sawa nitakusaidia. Lakini lazima ionekane kwamba amevamiwa na majambazi kwa sababu sisi hatuwezi kutibu mtu wa aina hii bila kuwa na PF3. Akipona na kueleza ukweli mtajuana huko wenyewe. Nitapiga simu kwa askari polisi mmoja rafiki yangu sasa hivi atatusaidia kupata PF3. Ila hakikisha kwamba kesho kabla ya saa sita unaleta chai kidogo kwa sababu ya huyo askari ya huyo askari. Shilingi laki moja inamtosha."

"Hamna taabu... Lakini unadhani atapona vizuri kabisa," akauliza Chris uso wake ukizidi kukunjuka kwa matumaini.

"Hopefully, atapona lakini ninachoweza kusema ili mgonjwa kuwahi kutoka hospitalinin kunategemea namna ubongo wake ulivyoathitika kutokana na kutikiswa na kipigo.

Chris alirejea Lemon Tree na kuamua kuondoka na mwanae kwenda kulala naye nyumbani kwake baada ya kumchukua kutoka kwa mhudumu.

Alijua yatakuwa maneno kwenda kupanda naye kwenye kitanda alichokuwa amelala Joyce.

***

Chris alishituka kutoka usingizini na kugundua kwamba mwanae Huba ndiye aliyemwamsha.

Aliangalia wakati kupitia kwenye simu yake na kugundua kwamba ilikuwa inaelekea saa nne asubuhi.

"Huba, umeamka. Haya mwanangu, nawa uso haraka nikupeleke kwashangazi yako."

"Baba namtaka mama. Mama yuko wapi?" Alihoji yule mtoto.

"Mama yuko kwa shangazi yako anakusubiri." Chris alitoka na Huba kuelekea bafuni.

Alimwogesha mwanae kisha akarejea naye chumbani na kumvalisha nguo tayari kwa kumpeleka kwa dada yake.

Muda wote alikuwa akitafuta maneno ya kumweleza dada yake akawa bado hajapata pa kuanzia.

Alimwacha mwanae akicheza kitandani, akaingia bafuni kujimwagia maji. Baada ya kuvaa nguo za kutokea siku hiyo alimchukua mwanae na kutoka naye sebuleni tayari kwenda kwa dada yake, Mwalimu Misango. Mpaka muda huo alikuwa hajajua atamweleza nini dada yake.

"Kwa jinsi anavyompenda Mama Kenny nitaanza kwa kudai ninataka kubadilika, niachane na Joy kwa afya ya ndoa yangu. Halafu nitamweleza kilichotokea nikijifanya kimenigusa sana. Atanielewa," alijisemea.

Wakati anakaribia mlango wa kutoka nje akiwa amemshika mwanawe, hodi ikasikika.Chris, akasita kidogo akisikilizia. Hodi ikagongwa tena. Akaenda kufungua.

Akakutana mlangoni na dadaye, Mwalimu Misango akiwa na kaka yake Mama Kenny, Yakob pamoja na baba mkwe wake yeye Chris. Akasikia moyo unafanya pa.

**Itaendelea...**

## VITA VYA ISRAEL, HAMAS:

# Waandishi 31 wamekwisha uawa

**YERUSALEM, Israel**



TAKRIBAN waandishi wa habari 31 wameuawa wakiripoti mzozo kati ya Israel na Hamas, kwa mujibu wa hesabu ya hivi punde kutoka kwa Kamati ya Kulinda Waandishi wa Habari (CPJ).

Kati ya waliopoteza maisha, 26 walikuwa Wapalestina, wanne Waisrael na mmoja wa Lebanon. waandishi wengine wanane wameripotiwa kujeruhiwa, huku tisa wakizingatiwa kutoweka au kuzuiliwa, CPJ imesema.

"Waandishi wa habari huko Gaza wanakabiliwa na hatari kubwa wanapojaribu kuangazia mzozo huo katika kukabiliana na shambulio la ardhini la Israel... mashambulizi ya anga ya Israel, kukatika kwamawasiliano na kukatika kwa umeme," shirika hilo lilisema katika taarifa yake Jumatatu iliyopita.

Miongoni mwa waliofariki dunia ni Roshdi Sarraj, mtayarishaji filamu maarufu wa Kipalestina na Issam Abdallah, mpigapicha wa video kutoka Beirut wa Reuters, ambaye aliuawa karibu na mpaka wa Lebanon kwa kupigwa makombora kutoka upandewa Israel, kwa mujibu wa CPJ. IDF ilisema inachunguza madai hayo.

IDF pia iliambia Reuters na mashirika ya habari ya Agence France Press kwamba haiwezi kuwahakikishia usalama waandishi wao wa habari wanaofanya kazi katika Ukanda wa Gaza, baada ya kutafuta hakikisho kwamba wafanyakazi wao hawatadhuriwa na mashambulizi ya Israel, kwa mujibu wa Reuters.

# Netanyahu alaani video 'katili' ya Hamas ya mateka

WAZIRI Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, amelaani kama 'propaganda za kikatili' video iliyotolewa na Hamas inayoonesha mateka wa Israel waliotekwa wakati wa mashambulizi ya Oktoba 7, mwaka huu.

Kanda hiyo iliyotolewa Jumatatu iliyopita, inawaonyesha wanawake watatu wa Israel, mmoja wao akimsuta Netanyahu na kutoa wito wa kuachiliwa kwa mateka.

Hamas iliwakamata mateka wasiopungua 230 katika mashambulizi hayo na Waisrael wasiopungua 1,400 waliuawa.

Ni wanne pekee ambao wameachiliwa hadi sasa. Israel imeanzisha operesheni kubwa ya kijeshi huko Gaza, ikisema kuwa lengo ni kuangamiza Hamas na utawala wake katika eneo hilo.



Wizara ya Afya inayosimamiwa na Hamas, imesema takriban Wapalestina 8,000 wameuawa.

Video ya mateka hao ilitolewa na mrengo wenye silaha wa Hamas, Brigedi za Izzedine al-Qassam.

Hatujui chochote kuhusu hali ambayo video hiyo ilirekodiwa.

Ni mmoja tu wa mateka anayezungumza kwenye kamera katika klip nzima.

Wafungwa wa kivita na mateka wanalindwa chini ya sheria za kimataifa za kibinadamu na BBC haipeperushi nyenzo ambazo zinaweza kuwa zimerekodiwa kwa hali ya kulazimishwa.

Katika taarifa, Netanyahu alisema: "Hizi ni propaganda za kikatili za kisaikolojia za Hamas-Isis [kinachojulikana kama Dola la Kiislamu."

"Tunakumbatia familia. Tutafanya kila kitu kuwarudisha nyumbani watu wote waliotekwa nyara na waliopotea."

Pia aliwataja mateka hao kuwa ni Elena Trupanov, Danielle Aloni na Rimon Kirsht. Binti ya Bi. Aloni mwenye umri wa miaka mitano, pamoja na dadake na shemeji yake na binti zao mapacha wa miaka mitatu, pia walitekwa nyara Oktoba, mwaka huu.

Katika kikao na wanahabari Jumatatu iliyopita, babake Bi. Aloni alisema moyo wake "ulikuwa karibu kukoma kudunda" alipoona picha yake.

Alitoa wito kwa Amir wa Qatar, ambaye amehudumu kama mpatanishi mkuu katika mazungumzo ya mateka, "kufanya kila juhudi kuwarudisha nyumbani."

## ...akataa usitishaji wa vita

WAZIRI Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, amesema anataka kuweka wazi msimamo wa nchi yake juu ya kusitisha mapigano.

"Kama vile Marekani isingekubali kusitishwa kwa mapigano baada ya kulipuliwa kwa Bandari ya Pearl au baada ya shambulio la kigaidi la 9/11, Israel haitakubali kusitisha uhasama na Hamas baada ya mashambulizi ya kutisha ya Oktoba 7, mwaka huu," alisema

"Wito wa kusitishwa kwa mapigano ni wito kwa Israel kujisalimisha kwa Hamas, kujisalimisha kwa ugaidi,"

"Biblia inasema 'kuna wakati wa amani na wakati wa vita'," aliongeza:

"Huu ni wakati wa vita."

"Vita kwa mustakabali wetu wa pamoja. Leo, tunachora mstari kati ya nguvu za ustaarabu na nguvu za kishenzi." BBC.



## VITA VYA UKRAINE:

# Familia nzima yauawa kwa kupigwa risasi

**KYIV, Ukraine**

WATU tisa wakiwemo watoto wawili, wamepatikana wameuawa kwa kupigwa risasi ndani ya nyumbayao katika mji wa Volnovakha Mashariki mwa Ukraine unaokaliwa na Urusi.

Maafisa wa Ukraine wanasema wanaamini kuwa wanajeshi wa Urusi waliua familia nzima ya Kapkanet Oktoba 27, mwaka huu kwa kukataa kuwapa nyumba yao.

Wachunguzi wa Urusi wanasema washukiwa wawili wanaume wameshikiliwa, wakisema ni wanajeshi wa Urusi kutoka Mashariki ya Mbali.

Ukraine na Urusi zimeanza uchunguzi tofauti kuhusu shambulio hilo. Picha zimeibuka kwenye mitandao ya kijamii zikionyesha miili iliyotapakaa damu na risasi ikiwa vitandani, baadhi yao wakiwa bado wamefungwa wakikumbatiana.

Mwendesha Mashitaka wa Ukraine, Dmytro Lubinets, alisema Jumatatu iliyopita kwamba mikono ya Warusi yenye damu ilihusika katika mauaji ya Volnovakha.

"Kulingana na habari za awali, wakaaji hao wameua familia nzima ya Kapkanets, ambao walikuwa wakisherehekea siku ya kuzaliwa na walikataa kukabidhi nyumba yao wenyewe kwa wakaaji kutoka Chechnya," alisema kwenye telegraph.

Ofisi ya Mwendesha Mashitaka wa Donetsk inayodhibitiwa na Ukraine, ikitoa taarifa za awali, ilisema washambuliaji waliovalia sare za jeshi, waliipiga risasi familia hiyo baada ya ombi lao la kutaka kuondoka katika nyumba hiyo kukataliwa.

Watoto wawili waliozaliwa mwaka wa 2014 na 2018, walikuwa miongoni mwa waathiriwa, ofisi hiyo iliongeza.

Kamati rasmi ya Uchunguzi ya Urusi, iliwataja waliokamatwa kuwa wanajeshi wa Urusi kutoka Mashariki ya Mbali ya nchi hiyo, ambao walikuwa wametia saini kandarasi na Jeshi la Urusi.

"Kwa mujibu wa taarifa za awali, sababu ya uhalifu huo ilikuwa migogoro ya ndani," kamati ilisema katika taarifa yake.

# Katumbi ruksa kuwania urais DRC

**KINSHASA, DR Congo**

MAHAKAMA Kuu nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), imetupilia mbali kesi iliyotaka kumzuia mwanasiasa wa upinzani Moise Katumbi, kuwania urais kwa madai kuwa si raia wa nchi hiyo.

Kesi hiyo iliwasilishwa mahakamani na mgombea mwingine, Noel Tshiani, akidai kuwa Katiba ya DRC, hairuhusu uraia pacha kwa kuwa baba wa Katumbi alikuwa raia wa Italia.

Wakili wa Katumbi, Herve Diakiese, aliteta wakati wa kesi hiyo hapo juzi kwamba hakuna uthibitisho wowote ya kuwa mteja wake ana uraia mwingine zaidi ya ule wa DRC.

Katumbi, mfanyabiashara tajiri mwenye umri wa miaka 58 na Gavana wa zamani wa Jimbo la Katanga, anachukuliwa kuwa mmoja wa wagombea wakuu dhidi ya Rais aliye madarakani, Felix Tshisekedi, katika uchaguzi uliopangwa kufanyika Desemba 20, mwaka huu.

# Pasira Fayira mrithi wa Scola Miel anayemkataa Cindy wa Koffi

- Asema Cindy hawezi kuwa Malkia wa muziki wa Congo
- Anafuata nyayo za Tshala Muana, Mbilia Bel, Scol



**Na Petter Mwendapole**

YAPO majina yametamba, yapo majina yanaendelea kuishi kutokana na kazi zao, Diesee Mukangi, Mbilia Bel, Scola Miel, Abeti Masikini, Tshala Muana, Mpongo Love.

Hawa ni wamama ambao wamefanya makubwa katika muziki wa Zaire (Congo-Kinshasa) ambapo mmoja wao sasa ndio anatambulika kama mama wa Taifa la Kongo.

Huyu ni marehemu Elizabeth Modiakai maarufu kama Tshala Muana.

Pamoja na 'uchizi' wake jukwaani, Tshala Muana aliamua kujitosa katika ulingo wa siasa ambapo alikuwa bega kwa bega la marehemu Rais Laurent Kabila katika vita ya kumuondoa Mobutu Seseko madarakani. Lakini kati ya wanamuziki wanaosifika kunyanyua vipaji vya wanamuziki wa kike ni Mbenzu Ngamboni Boskili maarufu kama Abubakari 'Benz' Bozi Boziana ama Babu.

Historia yake inaanzia kwa kina Diesse Mukangi, Scola Miel, Betty Sumbu. Kama unakumbuka Tembe na Tembe, Mitshuri, Mela albamu kama Piere Noel Confience, uwezo wa wadada hao utaona wazi.

Jinsi alivyokuwa akiwapa nafasi wadada hawa...waliweza kwenda kujitegemea wenyewe lakini pia ilimpa hamasa Mopao Mokonzi, Koffi Olomide kumpora Scola kutoka Anti Choc na kumuweka Quartier Latin.

Japo kwa muda mfupi lakini kazi aliyoifanya iliendelea kubaki kichwani kwa Koffi na matokeo yake leo Cindy L'a coir anasimama jukwaani kama kiongozi wa bendi.

Safu ya burudani ya UELEKEO, ilipiga hodi mpaka Kinshasa, Congo kwa usaidizi wa mwanamuziki Alain Mulumba Kashama tulipata ua jipya katika muziki wa dansi wa Congo, Pasila Fayira binti wa miaka 29.

Katika mazungumzo na gazeti hili, Pasila anasema alianzia muziki kanisani na hasa kutokana na wazazi wake ambao walikuwa waimba kwaya.

"Nilianza kuimba kanisani na miaka Kumi iliyopita nikaona nafasi kwa Mzee Boziana ndio nikajiunga nae.

Tangu wakati huo nimesafiri nae sehemu mbalimbali ikiwemo Tanzania na kurekodi albamu na Twanga Pepeta kwa Mama Asha Baraka," anasema.

Mwimbaji huyo mnene kiasi ambaye sauti yake inarandana na Scola anasema kuingia kwake katika muziki kulichangiwa na wakongwe waliotajwa pale mwanzo. Amesharekodi albamu mbili na gwiji huyo wa muziki Afrika.

"Albamu ya kwanza ilikuwa inaitwa Fiko Fiko na albamu ya pili inaitwa Tout History ambapo natarajia pia kuweka wimbo wangu."

Katika wimbo ambao uliachiwa kwanza wa Fleur de lys, Pasila ametamba vilivyo kwa kuimbisha wimbo wote. Albamu ya Tout History ilikuwa mtaani rasmi Novemba 18 mwaka 2017.

Pamoja na wazazi wake kuimba kanisani lakini dada yake mkubwa Hellen Fayila alikuwa mwimbaji wa TP OK Jazz enzi ya Franco huku kaka zake wako Marekani na mara moja moja huwa wanaimba.

Pasira anatoa mtazamo wake kuhusu Cindy La Coeur wa Koffi Olomide ambaye kwa sasa anachukuliwa kama ndiye Malkia wa dansi Congo.

" Ni mwanamuziki wa kawaida ila amepata bahati kuwa kiongozi wa bendi yake lakini hana kitu cha kutisha na hawezi kuitwa malkia wa muziki wa Congo kwa sasa. Kuhusu mikakati yake ya baadae amesema atatengeneza nyimbo na mmoja watu waliomfanya aingie katika muziki ingawa hajajua ni yupi kati yao atakayeimba nae. Pasila anayetoka katika familia ya watoto tisa, wa kike wakiwa watano na wakiume wanne, hajaolewa na wala hana mtoto.

***Wiki ijayo kwanini Empire Bakuba haikuendelea baada ya kufariki Pepe Kalle, Bileku Mpasi, Elvis Kunku, Gode Lofombo wanazungumza na Uelekeo nini kilitokea USIKOSE***

# Makocha wa soka na mitindo ya mavazi

**Na Valensi Mbaga**

BURUDANI ya soka sio tu uwanjani lakini hata katika muonekano hasa wa walimu wa timu. Wapo makocha ambao wanaongoza kwa unadhifu hasa wakiwa uwanjani. Kwa aina ya pesa katika soka, hakuna sababu ya kuwafanya wasimamizi kuonekana kuvaa vibaya.

Msimu wa Ligi Kuu ya 2023-24 umeanza, na timu mbalimbali zimeshajiweka mahali pazuri. makocha baadhi wametisha zaidi msimu huu kutokana na unadhifu wao na wafuatao ni wale waliotisha zaidi misimu kadhaa iliyopita hadi sasa na bado wamesimamia umahiri wao.

**10. Luis Enrique**

Enrique anaeleweka sana kama kawaida akiwa na Uhispania kama kocha nadhifu na mwenye muonekano mzuri wa kimavazi.

Akipeleka mitindo katika ulingo wa kimataifa, Luis Enrique anapongeza falsafa yake ya kuvutia na yenye subira ya soka kwa mtindo wa hila lakini wa kuthubutu. Haogopi kujiondoa kwenye uvaliaji wa suti na mara kwa mara na kupenda kuonekana katika suruali fupi isiyogusa kifundo cha mguu na chini kuvalia sneakers na fulana au sweta na mara nyingi huwa za bei ghali.

**9. Sinisa Mihajlovic**

Mihajlovic alipenda kuvalia Air Jordan katika mitoko mbali mbali. Si tu kwamba yeye ni meneja mzuri na mpiganaji kamili, Sinisa Mihajlovic humshinda kila mtu ambaye anashiriki mawasiliano naye.

Mara nyingi, Mihajlovic anapenda kutinga T-shirts i na jumper, hujifunika baridi kwa scuff laini, glavu za ngozi na kofia ambayo ni wachache sana wangevaa. Uvaaji wake ni kama Icing kwenye keki, kwani unapambwa sana na mkusanyiko wake wa viatu. Meneja huyu wa Bologna ana mkusanyiko mzuri wa viatu na ni maarufu akiwa ni mfuasi wa mavazi ya juu ya Off-White Jordan 1.

**8. Scott parker**

Aliekuwa meneja wa Fulham Scott Parker sasa anasimamia Club brudge anatajwa kuwa moja kati ya makocha watanashati zaidi.

Japo Scott Parker bado hajaongoza klabu yake kupata mafanikio mazuri ila 'je, yeye ni mzuri, au anavaa vizuri? Yeye amepita na kuongoza kwa rangi zinazoruka katika idara ya mitindo, ingawa. Huenda kusiwe na mtu mwingine kwenye sayari aliye na mzunguko bora, wa kipekee wa makoti mazuri kuliko Parker.

**7. Mikel Arteta**

Kocha mkuu wa Arsena,l Mikel Arteta amekuwa akiibadilisha timu hiyo kuwa muundo wake kwa misimu kadhaa sasa.Huku Mtindo wake mzuri wa mawazi umekuwa ukiwavutia wengi . Kwa kawaida mchanganyiko maridadi na ya busara kwa kuvalia suti huku akiwa na mwonekano mdogo sawa na amigo wake Pep Guardiola. Ni mtu ambaye bila shaka anaweza kuvuta wakufunzi waliopenda kuvalia suti kumuona kama mfano mzuri kwao.

**6. Jurgen Klopp**

Mjerumani huyu mwenye mizuka mingi uwanjani kama shabiki, Amejulikana kuvalia suti kwa nadra sana huku Akipenda kuvalia makoti ya gharama na bila kukosa kofia kichwani . Na hii inampa muonekano wa kipekee na kumuweka huru kufanya chochote uwanjani.Jurgen Klopp anafanana sana na mjerumani mwenzake Hans flick kwa namna ya uvaaji.



**5. Erik Ten Hag**

Muholanzi Erik Ten Hag anaonekana kuwa na pumzi mpya ya maisha kama meneja wa Manchester United. Huko nyuma alikuwa akipenda kuvalia koti jepesi na shati na kufanikiwa kuwa na muonekano kabambe kwa namna hii ya uvaaji wake .lakini itabidi tuone ikiwa yeye ni meneja wa suti au tracksuit katika misimu kadhaa ijayo.

**4. Cesare Prandeli**

Mwonekano wa kipekee wa Kiitaliano unakamilishwa kwa karibu zaidi na si mwingine ila Cesare Prandelli na ndiyo maana anashika nafasi ya nne katika orodha yetu ya wasimamizi wa soka waliovalia vizuri zaidi.

Ni mara chache sana utamuona akiweka mguu vibaya linapokuja suala la kuvaa suti zilizotengenezwa kikamilifu. Meneja huyo wa zamani wa Italia, wakati wake akiwa Fiorentina, mara nyingi alikuwa na ujasiri na kuunganisha suti yake na kitu cha zambarau ambacho kilikuwa rangi ya klabu. Wakati mwingine alikuwa akivaa shati ambalo lingekuwa jeupe









na suti nyeusi kabisa ambayo ingemfanya mtu afikiri kwamba suti hiyo ilibuniwa kwa ajili yake na yeye peke yake. Mwonekano wa Prandelli ni wa kitambo na hakuna mtu anayeweza kukaribia ukamilifu wa mtindo ambao Prandelli anauonyesha kando.

**3. Roberto De Zerbi**

Roberto De Zerbi ameleta mtindo wake wa Kiitaliano nje ya uwanja, na mtindo wa soka juu yake. Kila mara huonekana maridadi na huvaa nguo nadhifu au nadhifu za kawaida. Hupendelea kuvalia sweta maridadi na viatu vikali vya kampuni mbali mbali maarufu.

**2. Eddie Howe**

Eddie Howe na Geordies wanapigana pande zote msimu huu, na kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa kwa mara ya kwanza katika takriban miaka 20. Mtindo wa Eddie unatokana zaidi na mtindo wa mjengo wa suti, ambao tunapenda kuuona katika dimba la St. James' Park kwa wakufunzi mbali mbali .

**1. Pep Guardiola**

Josep 'Pep' Guardiola amekuwa mtu maridadi bila kujali amekuwa klabu gani. Kutoka Barcelona hadi Bayern na sasa Man City, anaweza kuvaa suti na shati, kuunganisha

**Ni mara chache sana utamuona akiweka mguu vibaya linapokuja suala la kuvaa suti zilizotengenezwa kikamilifu. Meneja huyo wa zamani wa Italia, wakati wake akiwa Fiorentina...**

na kupata mchanganyiko mzuri, na ni mfuasi wa kuvalia viatu vya kahawia.

Pia anajulikana kwa kuvalia mashati ya mikono mifupi na bado kuwa na muonekano mzuri sana na pia usimamizi wa timu. Pep anaweza kuchanganya mtindo ya aina mbali mbali na kuonekana mahiri sana na anaonekana kuwa nadhifu kila wakati.

Unadhifu wa makocha hawa pia unaendana na ubora wa timu zao kwani wote wanafanya vizuri katika ligi zao na kuzalisha vipaji vingi katika timu hizo.

# Ballon D'or yaenda kule kule

PARIS,Ufaransa.

BAADA ya kukamilika kwa droo ya Ballon d'Or , wachezaji mbali mbali wameibuka vinara wa tuzo hiyo.

Mshambuliaji wa Argentina na Inter Miami Lionel Messi ameshinda tuzo ya Ballon d'Or kwa Wanaume kwa mara ya nane.Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 alitambuliwa katika sherehe hizo mjini Paris baada ya kuisaidia nchi yake kushinda Kombe la Dunia nchini Qatar mwaka jana.

Messi alishinda tuzo yake ya Ballon d'Or iliyoongeza rekodi yake

**Ni heshima kuwa mbele ya baadhi ya wachezaji bora zaidi duniani hapa na baadhi ya bora kuwahi kucheza mchezo huo. Kushinda tuzo hii...**

mbele ya mshambuliaji wa Manchester City Erling Haaland. Fowadi wa Ufaransa Kylian Mbappe ambaye amekuwa mtu wa pili kufunga hat-trick ya mwisho ya Kombe la Dunia katika kupoteza kwa penalti 4-2 dhidi ya Argentina alimaliza wa tatu.

"Ni vizuri kuwa hapa kwa mara nyingine tena kufurahia wakati huu," Messi alisema. "Kuweza kushinda Kombe la Dunia na kufikia ndoto yangu." Nyota huyo wa zamani wa Barcelona na Paris St-Germain aliongeza:

"Sikuweza kufikiria kuwa na kazi ambayo nimekuwa nayo na kila kitu ambacho nimefanikiwa, bahati ambayo nimepata kuwa sehemu ya timu bora zaidi katika historia."

Huku Kiungo wa kati wa timu ya taifa ya Uingereza na Real Madrid, **Jude Bellingham** amechukua tuzo ya mchezaji bora wa dunia mwenye umri wa chini ya miaka 21. Jude alionyesha kiwango bora sana toka msimu uliopita na kupelekea kushinda tuzo hiyo.

Pia aliisaidia England kufika robo fainali ya Kombe la Dunia nchini Qatar.Bellingham alichaguliwa mbele ya Jamal Musiala wa Bayern Munich, huku washindi wa zamani wenzi wa Barcelona Gavi na Pedri pamoja na mchezaji mwenza wa Real Eduardo Camavinga pia kuwania tuzo hiyo.

Alisema: "Ni orodha kubwa ya wachezaji [waliowahi kushinda tuzo hii kabla]. "Ni heshima kuwa mbele ya baadhi ya wachezaji bora zaidi duniani hapa na baadhi ya bora kuwahi kucheza mchezo huo." Kushinda tuzo hii kunamaanisha mengi lakini kwangu jambo muhimu ni mataji ya timu na jambo muhimu kwangu ni kusonga mbele na kusaidia Real Madrid na England kushinda mataji kwa miaka mingi."








**Emiliano Martinez** atambuliwa kama golikipa bora zaidi duniani Mshindi wa Kombe la Dunia la Argentina na mlinda mlango wa Aston Villa Emiliano Martinez alishinda taji la Yashin Trophy kwa mlinda mlango bora zaidi duniani.

Martinez alishinda Golden Glove nchini Qatar, akiokoa mkwaju wa penalti kutoka kwa Kingsley Coman katika ushindi wa mikwaju ya penalti dhidi ya Ufaransa kwenye fainali. Pia aliisaidia Aston Villa kumaliza nafasi ya saba kwenye Premier League na kupata nafasi ya kushiriki Ligi ya Europa Conference. Hata\ hivyo, Martinez alikejeliwa na baadhi ya watu waliohudhuria sherehe hizo za Paris. Kipa huyo alikosolewa kwa sherehe hii baada ya kushinda Kombe la Dunia dhidi ya Ufaransa mwaka jana.

Klabu ya **Manchester City** washinda tuzo ya klabu bora ya mwaka. City ilitawazwa klabu bora ya mwaka katika tuzo hizo kwa mwaka wa pili mfululizo. Kikosi cha Pep Guardiola kilikuwa timu ya pili ya Uingereza kushinda Treble ya Ligi ya Mabingwa, Ligi ya Premia na Kombe la FA msimu uliopita. Walikuwa na wachezaji saba walioteuliwa kuwania tuzo ya Ballon d'Or kwa wanaume.

**Vinicius Jr** alitambuliwa kama Mchezaji bora katika kupigana dhidi ya ubaguzi wa rangi .Winga wa Real Madrid Vinicius Jr alipokea Tuzo ya Socrates kwa mchango wake nje ya uwanja na aliapa kuendelea kuzungumzia ubaguzi wa rangi katika soka la dunia.

Vinicius amekuwa akilengwa na unyanyasaji wa ubaguzi wa rangi mara kwa mara katika michezo ya La Liga kwa misimu miwili iliyopita. Alitambuliwa kwa kuanzisha taasisi inayojenga shule katika maeneo maskini na kuwekeza katika elimu nchini Brazili. "Nitabaki imara katika vita dhidi ya ubaguzi wa rangi,"alisema Mbrazil huyo. "Ni jambo la kusikitisha sana kuzungumzia ubaguzi wa rangi siku hizi, lakini inabidi tuendelee kwenye mapambano ili watu wateseke kidogo."

# FIFA yamfungia Rubiales kwa 'denda'

**MADRID, Hispania**



RAIS wa Chama cha Soka cha Hispania, Luis Rubiales amefungiwa kujihusisha na soka kwa miaka mitatu na FIFA kutokana na tukio la kumbusu mchezaji kwenye fainali ya Kombe la Dunia la Wanawake.

Rais huyo alimbusu nahodha Jenni Hermoso mdomoni wakati wa hafla ya utoaji tuzo huko Sydney mnamo Agosti 20, wakisherehekea ushindi wa bao 1-0 dhidi ya England baada ya mechi.

Rais huyo alijaribu kuendelea na majuku yake kabla ya kulazimika kujiuzulu mwezi uliopita, kufuatia tuhuma hizo, na hivi sasa ameadhibiwa baada ya kukutwa na hatia ya kukiuka kifungu cha 13 cha kanuni za nidhamu za FIFA.

**Rais huyo alimbusu nahodha Jenni Hermoso mdomoni...**



# Khalid Abdalah ateuliwa Kombe la Dunia

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Soka Duniani (FIFA) limemteua Mtanzania Khalid Abdalah kusimamia mechi ya Kombe la Dunia.

Abdalah ni Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), ameteuliwa kuwa Kamishna wa mchezo kati ya Djibouti na Guinea Bisau.

Timu hizo zinawania Kufuzu Kombe la Dunia 2026 mchezo utakaochezwa Novemba 20, 2023 nchini Djibouti.

# Azam wameanza kujitoa

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI ligi ikiangia raundi ya saba inaonekana taratibu maji na mafuta yanaenda kujitenga.

Ni kama Azam wameanza kukata moto katika kuelekea mbio za ubingwa baada ya kukubali vichapo viwili mfululizo wakipoteza Dodoma Jiji wamendelea kuolsogea taratibu wakitafuta ukubwa wa Top Four.

Baada ya kupoteza mbele ya Yanga, Azam wakapokea kipigo kingine kutoka kwa Namungo wakitandikwa mabao matatu ikiwa na maana wamepoteza pointi nane ambazo kwa vinara Simba wao hawajui sare wala kufungwa.

Dodoma ambao juzi wameifunga JKT msimu uliopita walionekana kutoa upinzani latika ligi hiyo ingawa walikata moto mwisho.

Tabora na Mashujaa ambazo zimepanda msimu huu bado zinaendelea kujitafuta. Huku wakongwe Mtibwa, Kagera Sugar wapo kama hawapo, kwa maana wamekuwa na homa za vipindi. Mtibwa wanaburuza mkia, Kagera wako nafasi ya Saba Singida nao wanaugonjwa usioeleweka mpaka sasa wameshinda mechi mbili.

**Ni kama Azam wameanza kukata moto katika kuelekea mbio za ubingwa baada ya kukubali vichapo...**



# Sasa wamerudi kazini

**Na Wemaeli Mmaraba**

NI kama ladha ya Ligi Kuu inazidi kuongezeka baada ya baadhi ya wachezaji waliokuwa wamejeruhi kuanza kurejea kwenye majukumu yao.



Singida FG ndio wa kwanza kutangaza utimamu wa kikosi chake wawili kurudi mazoezini.

Nyota hao mlinzi Joash Onyango 'Babu' na Frank Mkumbo jana waliungana na wenzao baada ya kuwa nje ya uwanja kwa muda mrefu kutokana na majeraha.

Wakati Josh na Mkumbo wakiwa nje wa majeraha, Dickson Ambundo alikuwa msibani baada ya kumpoteza baba yake mzazi.

Kurejea kwa wachezaji hao sasa kunaifanya timu hiyo kuwa na uhakika wa machaguo zaidi katika mechi zinazofuata.

# Katumbi kuwania Urais Kongo

**Na Mwandishi Wetu**

MMILIKI wa klabu ya TP Mazembe na Gavana wa zamani wa Jimbo la Katanga, Moise Katumbi ambae anatarajiwa kuwania Urais kwa tiketi ya upinzani baada ya Mahakama Kuu chini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kutupilia mbali kesi iliyotaka kumzuia Katumbi kuwania urais kwa madai kuwa si raia wa Nchi hiyo.

Kesi hiyo iliwasilishwa mahakamani na mgombea mwingine Noel Tshiani akidai kuwa Katiba ya Kongo hairuhusu uraia pacha kwa kuwa baba wa Katumbi alikuwa raia wa Italia.



Wakili wa Katumbi Herve Diakiese aliteta wakati wa kesi hiyo hapo jana kwamba hakuna uthibitisho wowote ya kuwa mteja wake ana uraia mwingine zaidi ya ule wa Kongo.

Wafuasi wa Bw Katumbi walionekana wakisherehekea nje ya mahakama katika mji mkuu, Kinshasa, baada ya uamuzi huo.

Spoti
Leo yetu ndiyo kesho yetu
| Jumatano Novemba 1 - 7, 2023 |

# Filamu 230 zapita mchujo wa Tuzo

**Na Flora Bathromew**

FILAMU 234 kati ya 536 zimepita katika mchujo wa kwanza wa tuzo za Filamu Tanzania ambazo zitafanyika baadae mwaka huu.

Katika filamu hizo, imeelezwa kuwa filamu 204 zinatoka Tanzania, wakati filamu 30 zinatoka Afrika Mashariki.

Katibu Mkuu wa Bodi ya Filamu Tanzania, Dk.Kiagho Kilonzo alisema mwaka huu kuna ongezeko la filamu kwa asilimia 18 tofauti na mwaka jana.



Katika uzinduzi wa tuzo hizo uliofanyika hotel ya Golden Tulip, Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Greyson Msigwa, aliwataka wasanii kutokukata tamaa na kwamba serikali inafahamu changamoto wanazopitia na kuwataka kushirikiana.

Msigwa alisema serikali inaiangalia sekta hiyo kwa ukaribu na ndio maana ikaamua kutoa mikopo kupitia mfuko wa Utamaduni.

Tuzo hizo zinafanyika kwa mara ya tatu mfululizo tangu kuanza kwake zinadhaminiwa na Kampuni ya Azam Media kupitia Channel yake ya Sinema Zetu.

# Aziz Ki anatamba tu

**Na Valensi Mbaga**

KIUNGO wa timu Yanga SC , Stephane Azizi Ki ameshinda tuzo ya mchezaji bora wa mwezi Oktoba wa klabu hiyo ijulikanayo kama NIC PLAYER OF THE MONTH.

Aziz ki ameonekana kurudi kwenye ubora wake baada ya kile kinachoonekana akikifanya katika michezo kadhaa na kusimama kama mfungaji kinara katika kikosi cha wanajangwani. Ki ameifungia Yanga mabao manne Mwezi oktoba , hat-trick dhidi ya Azam FC kwenye ushindi wa 3-2 na bao moja alilofunga dhidi ya Geita Gold FC.

Ki anakuwa mchezaji wa kwanza kushinda tuzo hiyo mpya inayodhaminiwa na Shirikia la Bima ya Taifa (NIC) kwa kura za mashabiki na wanachama wa Yanga SC.

Na kwa sasa ndiye mfungaji kinara kwenye msimamo wa Ligi Kuu akiwa pamoja na Jean Baleke kutoka Simba SC ambao wote wana mabao sita.

NIC waliweka mezani milioni 900 kudhamini tuzo hizo.




# UVCCM, TVF wayajenga Dar

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi Taifa Fakii Raphael Lulandala (MNEC),*amkutana na kufanya mazungumzo na Viongozi wa Shirisho la Mpira wa Wavu Tanzania (Tanzania Volleyball Federation (TVF).

Kikao hicho kilichofanyika Ofisi Ndogo za Makao Makuu ya Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi Upanga Jijini Dar es Salaam.

Katika kikao hicho, wavu waliwakilishwa na Mwenyekiti Mhandisi, Magoti Mtani na Katibu Mku7 Laurance Safari.

Kikao hicho kiliangalia changamoto zao na kuzitafutia ufumbuzi, kutafuta namna bora ya kuufanya mchezo wa wavu kuwa fursa ya ajira kwa vijana kama ilivyo kwa mpira wa miguu na zaidi kudumisha Ushirikiano kati ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi na TVF ambao ni chanzo cha kukuza Vipaji vya Vijana wengi nchini.

Pamoja naye Katibu Mkuu alikuwa na Manaibu makatibu wakuu wa Jumuiya Mussa Mwakitinya (MNEC), Naibu Katibu Mkuu Bara na Mussa Haji Mussa, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar.



# Serikali ya Uingereza yatua Simba, Yanga

**Na Mwandishi Wetu**




BALOZI wa Uingereza nchini Tanzania, David Concar ametembelea klabu za Simba na Yanga katika kuhakikisha zinafanya vizuri katika majukumu yao.

Awali Balozi Concar alifika Uwanja wa klabu ya Simba maarufu kama Mo Arena uliopo Bunju.

Balozi huyo alikutana na benchi la ufundi na wachezaji wa Simba ambao jana walianza mazoezi rasmi kujiandaa na pambano dhidi ya Yanga.

Mara baada ya kutoka Bunju, Balozi huyo, alikwenda Makao Makuu ya klabu ya Yanga ambao alipokelewa na Rais wa wao, Mhandisi Hersi Said na kufanya kikao.

Simba atakuwa mwenyeji katika mechi itakayofanyika Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa.

Wekundu hao wa Msimbazi wamemkaribisha pia Kocha wa Yanga, Miguel Gamond ili akafuatilie mazoezi ya timu yao.

Katika mechi iliyofanyika juzi dhidi ya Ihefu, Gamond na benchi lake la ufundi walikuwa Uwanjani wakifuatilia mechi hiyo.

Kitendo hicho, kilimfanya Meneja Habari wa Simba, Ahmed Ally, kumkaribisha Gamond Mo Arena Bunju.

**Mara baada ya kutoka Bunju, Balozi huyo, alikwenda Makao Makuu ya klabu ya Yanga ambao alipokelewa...**